Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 72 No. 165 | RAJAB 1432 AH | JUNI 2011 | IHSAN 1390 HS | BEI TSH. 500

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Je, aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya utawa wa Mwenyezi Mungu na radhi (Yake), ni mbora au aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo unaopukutika udongo wake, ukaanguka pamoja naye katika moto wa Jahanamu? Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wadhalimu.

(At-Tawba, 9:109)

HadhratKhalifatulMasih(atba)awaambiaWaaminio

Niwajibukuitii Serikali iliyomo madarakani

Na Mwandishi wetu

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani Hazrat Mirza Masroor Ahmad (atba) amewataka waaminio waendelee kutii serikali zilizomo madarakani na wajiepushe kabisa na maandamano na ghasia zinazoendelea katika sehemu nyingi duniani kwa hivi sasa.

Kiongozi huyo wa kiroho amesema silaha peke yake anayoitumia yule anayemcha Mwenyezi Mungu ni maombi kwani Mwenyezi Mungu Ana uwezo wa kubadili hali ya mahangaiko kuwa ya utulivu.

Akigeukia jambo linalowasumbua waaminio, khususan hali ya ghasia zinazoendelea pembe zote za dunia na iwapo waaminio wanatakiwa kushiriki katika maandamano hayo, kiongozi huyo amesema hakuna haja yoyote ya mahangaiko kwani mafundisho ya kifanyike nini katika hali ya namna hiyo yametolewa na Qur'an Tukufu, Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w) na maelezo bayana yaliyotolewa na Masihi Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s).



Amirul Muuminuun (Kiongozi wa Ahmadiyya duniani - Hadhrat Mirza Masroor Ahmad - Khalifatul Masih V (atba)

Akifafanua mafundisho ya Qur'an Tukufu katika mnasaba huu kiongozi wa Ahmadiyya alinukuu aya ya Qur'an Tukufu ambayo husomwa katika hotuba ya ijumaa "Na Anakataza upujufu, na uovu na uasi" (16:91).

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ameeleza neno la kiarabu 'Baghyi' (uasi) kuashiria mvua kali ambayo inaharibu mazao. Huzur alieleza kuwa hii ina maana yule anayepunguza haki au anayezidisha katika haki iliyo halali, Mwenyezi Mungu Anakataza sehemu zote hizi mbili, anayeongoza na anayeongozwa wasichupe mipaka iliyowekwa na wakichupa basi watakuwa wamefanya kosa kwani hiyo ni mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu.

Akiendelea Huzur alisema katika hali tuliyo nayo kwa hivi sasa ni wananchi wanao chukua hatua kali zaidi dhidi

Endelea uk. 3

Darul Aman - Qadian

Na Mwandishi wetu

Hivi jamani ni furaha iliyoje na ufaulu kiasi gani ukijaaliwa kuwa katika chumba alipokuwa anafanyia maombi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ukavuta hewa ya mahala alipozaliwa. Wenye bahati hiyo ni wachache na miongoni mwa hao ni Mtanzania Mohamedi Yunus Haj aliyebahatika kubisha hodi katika kijiji alipozaliwa mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na Hakimu muadilifu Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s). Na kijiji chenyewe hicho ni Qadian.

Bwana Mohamed Yunus Haji alifunga safari ya kwenda India kwa munajili ya kuhudhuria nikah ya binti yake Shazma aliyeolewa na kijana wa Qadian Bw. Hamid.

Endelea uk. 4



Bw. Ghulam Qadir wa Qadian - mmoja wa Madarwesh waliobaki Qadian kwa ajili ya kuulinda mji huo wa Kihistoria - wakati bara Hindi ilipogawanywa kuwa India, Pakistan na Bangladesha ya leo, hapo mwaka 1948

Sheikh Mubarak Mahmood - Afariki dunia

Na Sheikh Fareed Ahmad, Tanga

Kwa masikitiko makubwa tumeondokewa na ndugu yetu mpendwa Sheikh Mubarak Mbashiri wetu wa Tanzania aliyefariki tarehe 04 May, 2011 Rabwah, Pakistan. *Ina lillahe waina ilayhi rajiuni.*

Yeye aliwasili Tanzania tarehe 21 April, 1998 . Baada ya kufika Tanzania alikaa miezi tisa Dar-es-Salaam chini ya Amiri na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Khan Sahib.

Baada ya Dar-es-Salaam alihamishiwa Arusha kama Mbashiri wa Mkoa wa Arusha na kwa kipindi hicho alitumwa Tarime Mkoa wa Mara kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa Msikiti.

Baada ya kumaliza alirudi katika kituo chake cha Arusha.

Baada ya kumaliza miaka mitatu Tanzania alipewa likizo kwenda Pakistan kupitia London.

Kwa hiyo katika safari hii



Sheikh Mubarak Mahmood

pia alipata bahati na baraka ya kuonana Khalifa na pia alishiriki katika Mkutano wa Mwaka wa Kimataifa mjini London. Baada ya kumaliza likizo Pakistan alirudi Arusha pamoja na familia yake.

Kutoka Arusha alipata uhamisho kwenda Tanga. Kipindi hicho yeye alitumwa

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SIO MTU BALI MFUMO

Mfumo wa dhulma, ukandamizaji na unyonyaji una desturi ya kutengeneza mashujaa au ukitaka magaidi ambao husimama kidete kutokomeza mfumo huo na hatimaye huwa alama ya harakati hizo za ukombozi.

Ingawaje mchango wa mtu binafsi ni muhimu katika kupambana na mfumo huo wa kidhalimu, ukweli unabaki ya kuwa ni mfumo unaoibua mashujaa au magaidi wa jamii na ili kuondoa mahangaiko na taharuki katika jamii dawa sio kumuangamiza yule shujaa au gaidi aliyetokana na maumivu hayo isipokuwa kuuteketeza mfumo unaosimama kwenye misingi ya ukandamizaji.

Kama kuna faida katika historia basi ni kutukumbusha yaliyowapata wale waliojaribu kuwaua mashujaa au magaidi na kwa hili tunaazima maneno ya mwandishi Shakespear katika mchezo wake Macbeth 'Tumemparua nyoka hatukumuua'. Kuua mwanaharakati au mpe jina lolote unalotaka ni kuahirisha tatizo na sio kupata ufumbuzi unaofaa.

Nani ambaye hafahamu kwamba Wajerumani waliwaua akina Kinjekitile, Mkwawa. Damu yao hiyo ndio imerutubisha mti wa uhuru wa Tanzania. Lobengura wa Matebele Zimbabwe alipewa msukosuko mkubwa hatimaye nchi hiyo ikapata akina Lobengura wengine nao wakatwaa mtutu wa bunduki na kuleta uhuru wa nchi yao. Dedan Kimathi alipambana vilivyo na walowezi huko Kenya lakini kifo chake hakikuzuia Kenya kujinyakulia uhuru wake.

Mfumo wa dhulma hauna budi kuangushwa bila kujali watawala wanamwita mtu yule anayeongoza mapambano jina gani. George Washington kiongozi wa mapinduzi ya Marekani alipewa majina mengi machafu na Waingereza. Nelson Mandela nani asiyejua kuwa alipewa shahada ya kuwa gaidi. Ukweli unabaki ya kuwa dunia kwa hivi sasa ina rutuba nyingi ya kuzalisha hao tunawaoita kuwa magaidi.

Mfumo wa kiuchumi ni wa kuwanufaisha watu wachache, wakati wengi wanaendelea kushinda kutwa bila kuweka riziki tumboni. Biashara inayoendeshwa ni kwa ajili ya kunufaisha mataifa fulani na waliobaki wanaendelea kuwa wachanja kuni na wateka maji kwa ajili ya wakubwa. Sauti za wanyonge zinazarauliwa na kupuuzwa. Wenye nguvu wanaweza kuwavamia na kuwaua na asiwepo yeyote wa kufurukuta. Upendeleo dhahiri wa baadhi ya mataifa kuwa wateule na wengine kuwa Kahungu ni mambo yanayoendelea kuumiza watu wengi.

Huyu anafaa kuwa na silaha za maangamizi lakini wewe hufai. Dunia iliyojengwa hivi isahau kabisa kupata amani. Utulivu utapatikana vipi? Furaha na vicheko vitapatikanaje? Lazima ikumbukwe ya kwamba furaha yoyote inayojitokeza kwa hivi sasa ni furaha ya muda. Binadamu anavumilia mateso kwa muda na lenye mwanzo lina mwisho.

Mali yote tunayoiona hapa duniani ni ya Mwenyezi Mungu. Sote bila ubaguzi ni viumbe wake, hakuna mwenye haki zaidi kuliko mwingine. Ni lazima tukumbuke kuwa tupo hapa duniani kwa muda mfupi na ukusanyaji wa mali kwa pupa haujawahi kumsaidia mtu yeyote. Kiburi na majivuno ndio chimbuko la maanguko.

Yakowapi madola yaliyoranda na kutamba na kuwafanya wengine watetemeke? Wako viongozi waliojitaja na kujivuna na wengine kutamka kadamnasi 'Mimi ni Taifa'. Wote hao wapo sasa katika kaburi la sahau kwa wale ambao bado ni wazima tungependa kuwakumbusha mistari ya dhahabu toka kwa Shaaban Robert:

Wako wapi waraibu, wa tambuu na popoo
Wenye sura za ajabu, kwa picha na kwa kioo
Na waliojihesabu, hawana makadirio
Kifo kimewaharibu, katika urembo wao.

Sheikh Mubarak Mahmood - Afariki dunia

Kutoka Uk. 1

ya kusimamia kazi ya ujenzi wa Mission House na Msikiti mjini Mtwara. Baada ya kukamilisha ujenzi alirudi Dar es Salaam. Basi aliyokuwaamepanda iliharibika njiani na pia barabara ilikuwa mbaya sana. Kwa hiyo sawa na usumbufu huo alifika Dar es Salaam usiku wa saa saba. Baada ya kurudi hakuoneysha wala hakulalamika ya kwamba yeye alipata tabu badala yake alionyesha subira na tabasamu.

Katika kipindi cha kila mkutano wa mwaka wa Tanzania alikuwa anapangiwa nafasi ya kuendesha mauzo ya vitabu na chakula. (Book stall na Food stall)
Alikuwa hodari wa kuendesha kazi hiyo na kila mwaka kazi hiyo ilileta faida kubwa sana chini ya usimamizi wake na ndio sababu Mbashiri huyu alikuwa anapangiwa kazi hiyo kila mwaka katika kipindi cha mkutano.
Sheikh Bakari Abedi Kaluta Sahib anaeleza ya kwamba Sheikh huyu alikuwa hodari na mahiri sana katika kutafuta hoja tena kwa haraka sana. Mimi sijapata tabu hata kidogo katika kutafuta hoja vipindi vyote nilipouwa na Mbashiri huyu katika muhadhara na mjadala.
Sheikh Bakari Abedi Kaluta Sahib anaendelea kueleza ya kwamba mwaka huu 2011 mimi na Dr. Iddi Mwanga tulitembelea Pakistan hasa tulienda kwa kuonanana Sheikh huyu nyumbani kwake.
Katika matembezi hayo alifurahi sana. Furaha na tabasamu ilionekana katika uso wake.Na mara kwa mara alisema Ahsante sana kwa kunitembelea na kuulizia hali yangu.
Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masihi wa tano a.t.b.a amesema katika hutuba ya Ijumaa tarehe 13 Mai, 2011 kuhusu Sheikh Mubarak Mahmood ya kwamba:
"Mbashiri wetu Mubarak Mahmood alifariki tarehe 4 May, 2011 baada ya kuugua kwa muda mrefu. Alikuwa na umri miaka 42. *Ina lillahe waina ilayhi rajiuni*. Mwaka 1989 alimaliza masomo yake. Aliitumikia Jumuiya kwa miaka 9 katika Jumuiya za Pakistan.Baadae mwaka 1998 alifika Tanzania. Akiwa Tanzania aliugua maradhi ya Saratan kisha alirudi Pakistan kwa ajili ya kupata matibabu. Katika Wakalat Tasneef alihudumia Jumuiyya katika Swahili Desk, na alivumlia sana katika maradhi yake. Maradhi haya ya Saratani ni yenye maumivu sana lakini alionyoshea subira sana katika hali hiyo. Alikuwa na tabasamu na alikuwa anakutana na watu kwa bashasha. Alikuwa Musi. Ameacha mke na mabinti wa 3 na vile vile ameacha wazazi. Ameaacha ndugu wa 4. Na yeye ni mtoto wa Seifu Ali Sahib ambaye ni Amir wetu wa Ameerpur Khas na vile vile ni mpwa wa Hydar Ali Zafar Sahib ambaye ni mbashiri wetu wa Ujerumani"
Mwenyezi ailaze roho ya marehemu Sheikh Mubarak Mahmood, mahali pema, peponi - Amin.

Salamu toka kwa Sheikh Durrani

Na Mwandishi wetu.

Kupitia Mtandao wa kijamii Sheikh Muzaffar Ahmad Durani ameendelea kuwakumbuka

Ndugu zake wa kiroho aliyewahi kuishi nao kwa wema hapa Tanzania. Akimtumia salamu za pekee kwa Mhariri wa gazeti hili la Mapenzi Ya Mungu na Waahmadiyya wote kwa ujumla aliwataka watu waendelee kuwakumbuka katika maombi yao ili kazi ya dini ipige hatua kubwa zaidi.
Akielezea hali ya Jamaat nchini Pakistan Sheikh Durran alisema, Sisi huku tuna vitu vingi vya kufanya tabligh ila tunakosa uhuru wa kutangaza imani yetu kwa sababu ya chuki ya watu na ambao wanaungwa mkono na Serikali ya Pakistan.
Sheikh Durran alitaka kujua maendeleo ya Shule ya Sekondari Ahmadiyya Kitonga na baada ya kumueleza hali ya shule alionyesha furaha na kuendelea kuahidi kuungana nasi kwenye maombi ili shule yetu iende mbele zaidi.
Alieleza kifo cha Sheikh Mubarak Mahmood na tayari ameandika habari hiyo kwenye gazeti la Al Fazl na ameituma kwa ajili ya Mapenzi Ya Mungu.
Katika salamu zake Sheikh Durran ambaye atakumbukwa na Waahmadiyya na maadui wa Ahmadiyya wa hapa Tanzania kwa jinsi alivyokuwa mahiri katika mihadhara mbalimbali amesema kuwa anahitaji sana kuandika makala kwa ajili ya Mapenzi ya Mungu lakini muda wake ni mdogo sana. Ameomba tumuombee zaidi ili apate nafasi ya kuandika. Alimalizia.



Sheikh MuzaffarAhmad Durrani

Mzee Abdulrahimu Nasibu Hija Katutoka

Na Mahmood Hamsin Mubiru, Dar es Salaam

Siku ya Jumatano tarehe 25/5/2011 tulikabiliana na Dr. Kitabu Pazi tukutane hospitali ya Mwananyamala milango ya saa kumi ili kumjulia hali Bwana Abdulrahimu Nasibu Hija ambaye alikuwa amelazwa. Ingawaje tulipotezana kidogo na Dr. Kitabu lakini baada ya muda kidogo tulionana na tukaongozana kumuona Bw. Nasibu. Kitandani tulimkuta binti yake Basibu na mkewe Bi mariamu Maliki. Dr. Kitabu aliinama kidogo na kumuambia Bw. Nasibu, 'nimekuletea Muadhama'. Aliinua macho kidogo na kwa tabasamu kubwa na furaha sana tulipeana mikono huku akionesha furaha. Nilimuuliza hali yake na akanieleza kuwa alikuwa anaendelea vizuri. Ingawaje alionesha hamu kubwa ya kuendelea kuzungumza niliona si vizuri kuendelea kumsumbua. Mara aliingia bw. Kassim Maftah baye akamjulia hali. Mipango ilifanywa ya kumpelekea Muhimbili na siku ya Jumatatu tarehe 30-05-201 tupipata habari ya kwamba bw. Abdulrahimu Nasibu Hija ametutoka. *Inna lilahi wainaa Ilaihi Rajiuun.*
Nilifahamiana na Bw. Nasibu Hija miakla ya sitini nilipokuwa ninasoma nay eye akiwa



Bw. Abdulrahim Nasibu (kushot o) akiwa kwenye picha ya pamoja na Bw. Mahmood Hamsin Mubiru katika ofisi ya Mapenzi ya Mungu siku ya sherehe za kukabidhiana jukumu la uhariri wa gazeti la Mapenzi ya Mungu

Endelea Uk. 7

Ni wajibu kuitii Serikali iliyomo madarakani

Kutoka Uk. 1

ya serikali zao. Akielekea upande wa Hadithi Huzur alisema ya kwamba hata kama kiongozi huyo hayuko sahihi wananchi wanatakiwa wawe na subira.

Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alisema; baada yangu kutakuwepo na ukosefu wa haki, unyanyasaji na wengine watapendelewa zaidi ya nyinyi. Mtaona mambo ambayo hamtakubaliana nayo. Alipoulizwa la kufanya katika hali ya namna hiyo, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alisema; wapeni haki zao viongozi na muombeni Mwenyezi Mungu juu ya haki zenu. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) pia alisema mtu yeyote asiyekubaliana na jambo lililofanywa na kiongizi wake anatakiwa awe na subira na yeyote anayemuasi kiongozi atakufa kifo cha kijahili.

Mtu alikuja kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) akilalamikia kiongozi aliyechaguliwa na Mtume (saw) na kusema kwa nini hakuchaguliwa yeye? Akimjibu Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alisema; Nitakapoondoka watu wengine watapewa kipaumbele kuliko nyinyi. Mnachotakiwa ni kuwa na subira hadi siku ya kiyama. Mtukufu Mtume Muhammad aliulizwa watu wafanyeje ikiwa kiongozi mwenye dhuluma amelazimishwa kwao? Alikataa kujibu. Aliulizwa tena na tena hakujibu. Alipoulizwa mara ya tatu akajibu kuwa hata katika hali hiyo kiongozi anatakiwa atiiwe. Kiongozi ataulizwa juu ya wajibu wake na anayeongozwa ataulizwa pia. Kuna wakati Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alichukua Baiat baada ya hapo alisema; ikiwa mtu amefanywa kuwa kiongozi asiulizwe ulizwe isipokuwa akifanya kufuru hadharani na katika hili watu wawe na ushahidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Akieleza mtizamo wa Wahabi kuhusu uongozi, Khalifa Mtukufu alisema Wahabi wana msimamo mkali katika hili. Wao wanasema ile kifuru ya kiongozi ikiwa bayana basi ni sawasawa kuangamiza uongozi wake. Pia wanakwenda mbali kidogo kwa kutangaza kuwa wale wasio waita makafiri wale waliotolewa fat'wa ya ukafiri wao pia makafiri. Huzur alisema kiini cha hadithi hiyo aliyoisoma hapo juu ni utii na wala haizungumzii uasi.

Akizungumzia juu ya jumuiyya ya Ahmadiyya na mahala panapoonyesha kutotii ni hali inayojitokeza katika Pakistan. Katika Pakistan Waahmadiyya hawaruhusiwi kujiita Waislam, kusoma Kurani Tukufu, kusoma kalima na kutoa Assalaam Alaikum. Hili ni jambo la dini na hivyo hatuna sababu ya kuonesha utii katika hilo. Kwa hakika sisi hatuasi na tunatii sheria nyingine za nchi. Kuhusiana na suala hili kiongozi wa Ahmadiyya alimnukuu Imam Nawawi Mwenyezi Mungu awe radhi naye kwa maelezo zaidi ya hadithi hiyo yeye Imam Nawawi alikuwa amesema kwamba kufuru hapa inamaanisha dhambi na akaendelea kusema kwamba jambo lolote baya likionekana katika serikali jambo lielezwe kwa ukweli lakini pasiwepo na uasi hata kama serikali yenyewe ni ya ukandamizaji na uonevu. Huzur alisema kinyume cha hivyo hivi leo pande zote zimo katika mgogoro na Muislam anamuua Muislam mwingine.

Akifafanua jambo hilo kwa upana zaidi kiongozi wa Ahmadiyya alinukuu hadithi ifuatayo; Mfano wa wale wanaofuata mipaka ya Mwenyezi Mungu na wale waliochupa mipaka hiyo wanafananishwa na watu waliokuwa katika mtumbwi. Baadhi walikaa juu na wengine chini. Waliochini walipotaka maji ilibidi wapande juu. Na hii iliwapa usumbufu walio juu. Mtu mmoja miongoni mwa wale waliochini alianza kutoboa mtumbwi, watu waliokuwa juu walianza kumuuliza anafanya nini? Yeye alijibu mimi ninapokuja juu kuchukua maji ninawapa usumbufu, na mimi siwezi kuishi bila maji. Hivyo waliyopo juu wakimkataza watamuokoa yeye pamoja na wao wenyewe ili wasizame. Huzur alisema watu wengine wanasema kutokana na kisa hiki kuwa wale wanaofanya uovu wakikatazwa kwa nguvu hatua hiyo si sawasawa, inaongeza uasi. Huzur alisema kuwa tukielewa kuwa hii inaashiria uasi dhidi ya dola basi ni kinyume na maneno ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w). Hadithi hapa maana yake ni kwamba inakubalika kuzuia ghasia, wala hiyo haihusu dola.

Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) asingeweza kusema jambo lolote kinyume na Kurani Tukufu. Aliwahi kusema ukiona kitu ambacho sio kizuri ukiondoe kwa mkono wako, na kama huna nguvu ya kuondoa jambo hilo kwa mkono basi liondoe kwa maneno na kama huna uwezo na hilo liondoe kwa kuchukia moyoni na hiyo ni imani dhaifu.

Akitolea ufafanuzi juu ya hadithi hii Huzur alimnukuu Imam Mullah Alikali ambaye alieleza hadithi hii kuwa; kuondoa jambo kwa mkono ni kwa ajili ya viongozi, na kuhusu maneno ni kwa ajili ya wasomi (Mamullah) na kukasirikia ovu hiyo ni kwa ajili ya umma wa waaminio. Huzur alisema haya ni maelezo mazuri ya hadithi. Na kuhusu hadithi iliyotangulia ya mtumbwi na wale walio na madaraka wenye mamlaka ya kuwakataza wengine. Kila mtu akianza kuzuia basi fujo itatokea na Kurani Tukufu inakataza hilo. "Na Mwenyezi Mungu Hapendi uharibifu" (2:206). Na kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba Mwenyezi Mungu hapendi "Na Anakataza upujufu, na uovu na uasi" (16:91).

Huzur alisema; tuna mifano ya Manabii na utii wao kwa dola. Hadithi inaeleza ya kuwa Manabii 124,000 walikuja duniani. Kurani Tukufu inaeleza ishirini hadi ishirini na tano na hakuna hata mmoja katika mitume hao aliyesema lolote kinyume cha kiongozi wa nchi katika mambo yaliyohusu kidunia au kufanya maandamano. Huzur akiendelea kufafanua juu ya Nabii Yusuf (a.s) alisema kuwa sura Yusuf (12) inaeleza juu ya Nabii Yusuf (a.s) na kwa ufupi ni kwamba yeye alikuwa waziri wa hazina katika serikali ya kipagani ya Mfalme wa Misri aliyekuwa na lakabu ya Farao.

Na kama Mfalme angelijua kuwa Nabii Yusuf (a.s) siyo mtiifu kwake na mnafiki Mwenyezi Mungu Apishe mbali, katu asingemchagua kuwa waziri. Na kwa hakika ni utovu wa nidhamu hata kuwa na wazo kuwa Nabii Yusuf kuwa ni mnafiki Mungu Apishe mbali. "Sheria ya Misri haikumruhusu ndugu ya Yusuf kukaa Misri. Hivyo Mwenyezi Mungu Alitaka na akaweka kikombe cha Mfalme katika mzigo wa ndugu yake, na upekuzi ulipofanywa kikombe kilikutwa katika mzigo wa ndugu yake (12:77). Hii inaashiria kuwa Nabii Yusuf alikuwa mtiifu kwa serikali ya kipagani nakushirikiana lakini hakumtii katika mambo ya dini.Mwenyezi Mungu Anaeleza katika Kurani Tukufu (4:60) Enyi mlioamini mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume wake na wale wenye mamlaka juu yenu, na kama mkigombana juu ya jambo lolote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora.

Akifafanua aya hii Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema; aya hiyo inatufundisha kuwa tumtii Mwenyezi Mungu, Nabii na walio na madaraka juu yetu. Pia alisema Enyi Waislam mkiwa na tofauti miongoni mwenu, pelekeni jambo hilo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa ajili ya uamuzi kama mnaamini katika siku ya Mwisho basi chukueni njia hii kwani hayo ndio maelezo yaliyo bora.

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani alieleza kuwa hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake kama ilivyoelezwa awali sio kuasi, hata hali iwe mbaya kiasi gani ya kidunia.

Masihi Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s) alisema; Kurani Tukufu inasema , Mtii Allah na wale walio na madaraka juu yenu. Kama mtu atasema kuwa serikali haipo hapa ni kosa lake. Chochote kinafanywa na serikali ambacho kimo katika sheria kinahesabika katika mnasaba huu. Masihi anasema ya kwamba kama mtawala ni mkandamizaji usimpinge ila jisafishe wewe mwenyewe. Mwenyezi Mungu Atawapatia kiongozi mwingine au Atamfanya mcha Mungu. Matatizo yote yanayotupata yanatokana na mwenendo mbaya, ushauri wangu ni kwamba muwe mfano wa watu wema katika kila nyanja. Msipore haki ya Mwenyezi Mungu wala msipore haki ya binadamu.

Akielezea jambo hilo hilo Khalifa tul Masi wa Pili Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) alisema; baadhi ya Waislam kwa makosa wanasema kwamba aya hii inahusu tu viongozi Waislam. Hii alisema ni kinyume na Kurani Tukufu na la msingi hapa sio wale walio dini moja. Mwenyezi Mungu Anawaeleza wasioamini katika Kurani Tukufu (6:13) Je hawakuwafikieni Mitume toka miongoni mwenu? Hii sio lazima kwamba wanaotajwa hapa ni wale wa dini moja. Agizo hapa ni kuwatii watu wanaoongoza nchi. Kama kuna kutoelewana na dola basi jambo hilo liachwe mikononi mwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Khalifatul Masih wa Pili alisema ya kwamba; kisa kuhusu Yusuf (a.s) katika Kurani Tukufu ni uthibitisho ya kwamba ni muhimu kumtii kiongozi bila kujali dini yake.

Akigeukia katika hali inayojitokeza ya kutoelewana baina ya mtawala na mtawaliwa kiongozi wa Ahmadiyya bila ya kujali dini ya kiongozi, agizo la Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni; Nawaagizeni muwe na taq'wa na utii uwe njia yenu hata kama mtu mweusi ni kiongozi wenu. Wale watakaokuwepo wakati nimekwisha toka, watakuwa na kutoelewana kwingi, katika wakati huo fuateni mwenendo wangu na baada ae mwenendo wa Makhalifa wangu walioongoka, shikeni kwa nguvu zote kamba hii kama tunavyoshika kwa nguvu kitu tunapotumia meno na katu msiache kufuata njia yangu na ya Makhalifa wangu waliyoongoka. Kinachotakiwa ni kumtii kiongozi hata kama ni dhalimu, na maombi yatumike katika kumbadili kiongozi huyo. Waahmadiyya popote wanapokuwa wakumbuke masharti ya Baiat.

Sharti la pili linasema "Atajitahidi sana kujiepusha kabisa na kusema uwongo, wala hatatazama wanawake wala kufanya ufisadi, ufidhuli, hiyana na uasi, hatavikaribia vitendo vya namna hii, wala hatashindwa na tamaa mbaya za nafsi yake". Na sharti la nne linasema "tena hatawadhuru hususa Waislam na kwa ujumla viumbe wote wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya tamaa mbaya ya nafsi yake, si kwa mkono wake wala kwa ulimi na viungo vyake vingine".

Masihi Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s) alisema; kuchafua amani ni jambo baya kuliko hata kuua. Alisema kushiriki katika migomo katika vyuo ni kinyume na mafundisho yetu na ni kama kushiriki katika uasi. Khalifatul Masih wa kwanza Hazrat Maulvi Hakimu Nurudini (r.a) alisema ni jambo la msingi kwa Muislam kumtii Mwenyezi Mungu, Mtume wake na wale walio na madaraka juu yenu. Alisema kwamba kiongozi akifanya chochote kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu au yale ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) hapo mtu hatakiwi kuonyesha utii au njia nyingine aondoke na kufanya hijra.

Akiweka sawa wale wanaoulizia mikutano ya kuwaunga mkono watu wa Kashmir iliyotayarishwa na Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) na kuilinganisha na uasi. Kiongozi wa Ahmadiyya alisema jambo hili lilikuwa ni kuwapa haki watu wa Kashmir na haikuhusiana na fujo za aina yoyote. Katika hili alisisitiza juu ya uporaji wa mali za watu wa Kashmir ambapo kodi yote ilichukuliwa na kiongozi. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) alipoulizwa msimamo gani uchukuliwe kuhusu kugoma mwaka 1929, alisema wasishiriki, lakini washiriki katika mikutano ambayo imeruhusiwa na serikali. Alieleza ya kwamba maduka ya Ahmadiyya yaliyobaki wazi wenyewe walipigwa na kulazimishwa kuyafunga. Aliagiza kwamba askari wapewe taarifa na kama wako tayari kutoa ulinzi hapo maduka yanaweza

Endelea Uk. 4

Darul Amaan - Qadian

Kutoka Uk. 1

Ilikuwa ni furaha kubwa kwa Bwana Mohamed Yunus Haji kukanyaga katika mji wa Masihi Qadian ambao umeelezwa katika bishara za ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa. Bw. Haji aliwasili katika mji wa Qadian na kwa mshangao mkubwa alipokelewa saa 8 za usiku na watumishi wa Masihi walihangaika kushoto na kulia ili kumkirimu mgeni. Chakula kilikuwa tayari muda huo lakini Bwana Haji aliwaeleza kuwa tayari alishapata chakula. Hata hivyo hawakutulia hadi yeye mke wake na watoto watatu walipopata mahala pa kulala.

Undugu wanaoonyesha ndugu zetu wa Qadian ni hali ya juu. Saa 12 asubuhi watumishi hao wa Masihi walikwishagonga mlango wa Bwana Yunus wakitaka kujua ni vitafunio vya aina gani alivyokuwa anahitaji. Haya ni mapenzi ya ajabu yenye uwezo wa kuuvuta moyo.

Qadian ni mahala pa historia na kivutio kikubwa cha kila Ahmadiyya. Baitul Dua ni chumba alipokuwa anafanyia maombi Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ni mahali ambapo kila Ahmadiyya anayefika Qadian anakuwa na shauku ya kusali katika chumba hicho. Bwana Yunus alipata fursa hiyo adimu.

Kivutio kingine ni Mnara wa Masihi. Kuna hadithi ambayo inapatikana katika Muslim isemayo Mtukufu Mtume Muhamad (s.a.w) alisema kuwa Masihi Aliyeahidiwa atashuka kwenye Mnara mweupe Mashariki ya Damascus. Bishara hii inazungumzia ujaji wa mara ya pili wa Nabii Issa (a.s). Katika lugha ya kiarabu 'Minarat' ina maana ya wakati na mahali palipo na nuru. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) katika hadithi hii alikuwa na maana ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) atadhihiri wakati itakuwepo nuru duniani na umbali hautaficha kitu chochote kisionekane. Kwa maneno mengine Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ataona mambo ya mbali na watu wataweza kumuona kutoka sehemu za mbali. Hii ina maana Masihi Aliyeahidiwa atadhihiri wakati vipo vyombo vya usafiri. Na wakati huo utakuwa wakati wa mwanga. Watu watapata mwanga na hivyo hapatakuwa na haja ya upanga. Hili linathibitisha kauli ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) aliposema Masihi Aliyeahidiwa ataweka kando silaha.

Maneno mengine ya bishara yametimia neno kwa neno. Qadian mahali alipodhihiri Masihi Aliyeahidiwa ni mashariki ya Damascus. Neno Damascus linaashiria itikadi ya utatu uliozaliwa katika mji huo. Ni katika mji huo Paulo alipopata wazo la kuwa Yesu (Mungu Apishe mbali) alikuwa Mungu, Mshindi dhidi ya kifo kwa kuwa alipaa mbinguni.



Bw. Yunus Haji (wa mwisho kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa Majlis Ansarullah nchini India. Aliyesimama katikati ni Sadr Ansarullah wa India Bw. Kari Nawab Ahmad, waliosimama kulia na kushoto yake ni Manaib Sadr Ansarullah India. Wa mwisho kushoto ni mtumishi katika ofisi ya Ansarullah Qadian.

Hivyo ili kutimiza bishara kidhahiri Hazrat Mirza Ghulam Ahmad Masihi Aliyeahidiwa aliamua tarehe 28/05/1900 kutimiza bishara hiyo. Hivyo ulianza ujenzi wa mnara mweupe katika Qadian. Jiwe la msingi liliwekwa siku ya Ijumaa tarehe 13/03/1903. Jiwe liliwekwa na Masihi Aliyeahidiwa baada ya maombi ya muda mrefu. Madhumuni ya mnara huo yaliainishwa na Masihi Aliyeahidiwa katika sehemu tatu:

1. Kwanza Muazini atoe adhana kila siku mara tano -akitangaza kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.
2. Taa zinazong'aa ziwekwe juu ya minara ili ziondoe giza na kumulika dunia ili watu waweze kuelewa mwanga wa kimbinguni.
3. Saa iwekwe juu ya mnara ili iwaeleweshe watu juu ya wakati. Waelewe kuwa huu ni wakati milango ya mbinguni imefunguliwa na hakuna haja ya vita vya upanga.

HISTORIA FUPI YA QADIAN:

Majiji na miji mingi duniani inafahamika na kupata umaarufu kutokana na jiografia ya mahala au kuwa makao ya serikali, kituo cha vyuo vikuu, kitovu cha viwanda, vivutio vya kihistoria, lakini Qadian ni mji mdogo karibu na Amritsar katika jimbo la Punjab -India na umepata umaarufu kwa sababu ni mahala alipozaliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Masihi Aliyeahidiwa mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s) aliyezaliwa tarehe 13/02/1835.

Inasemekana ya kuwa Qadian ilianzishwa mwaka 1530 AD. Mirza Hadi Haiq ndiye alikuwa Hakimu wa kwanza wa sehemu hii. Kwa sababu yake eneo hili liliitwa Qadi Mirza Haiqi Baig. Hata hivyo kwa mapenzi yake makubwa juu ya Islam aliita sehemu hiyo Islamapur Qazi. Kadri muda ulivyokwenda sehemu hiyo ikaitwa Qazi Maji. Hatimaye ikawa Qadian. Ni katika mwaka 1834 wakati wa utawala wa Raja Ranjith Singh ndipo Qadian na vitongoji vyake vilirejea mikononi Mirza Ghulam Murtaza Ahmad -baba yake Mirza Ghulam Ahmad.

Katika kipindi hicho Qadian haikuwa na umaarufu wowote. Hapakuwepo barabara za maana wala hospitali wala kituo cha reli. Msomi maarufu wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Abdulrahim Dardi sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa aliyefanikiwa kumrudisha Qaidil Azim Mohamed Ali Jina katika siasa za Pakistan. Na mwandishi wa kitabu maarufu Ahmad akieleza juu ya Qadian alikuwa na haya ya kusema "Qadian kilikuwa ni kijiji kidogo chenye watu 1000 kilichozunguukwa na milango minne. Wakati wa mvua Qadian kilikuwa kama kisiwa na watu waliingia kwa mtumbwi". Naye sahaba mwingine wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) Mwanasheria maarufu na mwandishi wa vitabu Sir Muhammad Zafrullah Khan amesema katika kitabu chake Nurudin "Qadian ulikuwa mji mdogo na wakazi wachache, kituo cha karibu cha gari moshi kilikuwa ni maili 11, upatikanaji wa maji salama ulikuwa ni wa hatihati.

Mabadiliko makubwa hata hivyo yalipatikana toka mwaka 1876. Hakuna hata mmoja aliyefikiri kuwa Qadian utakuwa mji wa elimu na sababu ya kuenezwa kwa Islam ya kweli kama ilivyofundishwa na Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w).

Qadian imo katika moyo wa kila Ahmadiyya na mapenzi hayo yalidhihirika zaidi wakati wa machafuko ya mwaka 1947. Wakati lilipozaliwa taifa la Pakistan. Hakuna ambaye alikuwa tayari kuondoka Qadian. Walipolazimika wakaondoka lakini nyuma wakabaki Madaruweshi waliojitolea kulinda mahali patakatifu alipozaliwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s)

Bwana Mohamedi Yunus Haji alipata bahati ya kukutana na baadhi ya Madaruweshi hao ambao ni wapole na wenye furaha kubwa ya kulinda sehemu hiyo muhimu katika Historia ya Islam.

DARUL AMAN -QADIAN

Ni wajibu kuitii Serikali iliyomo madarakani

Kutoka Uk. 3

kufunguliwa au sivyo hapana. Alisema; migomo huleta hasara kwa wateja na wenye maduka na alisisitiza kwamba hatuwezi kushirikiana na wanaovunja sheria kwa sababu hiyo ni kinyume na dini yetu.

Hata Waahmadiyya wateswe vipi, sheria ya dini na sheria za nchi haziwezi kuvunjwa.

Kwa kumalizia kiongozi wa Waaminio alieleza ya kwamba, mwanzoni mwa hotuba yake alikuwa amenukuu (2:206) "Na Mwenyezi Mungu Hapendi uharibifu". Alisema aya hii inawaonya viongozi wabaya na wadhalimu. Kurani Tukufu haiwaoneshi njia umma tu, bali wanaoneshwa na watawala ikiwaambia kuwa wasiwe na majivuno kuhusu madaraka waliyo nayo na wasiwe wakatili. Kiongozi wa Ahmadiyya alisema; katika kilio kinachosikika kwa hivi sasa ni kile cha utumiaji wa fujo kwa rasilimali za taifa na wananchi kunyimwa haki zao. Ni bahati mbaya ilioje ya kuwa waliopewa madaraka na Mwenyezi Mungu wanayatumia vibaya kiasi hiki ya kwamba nchi inatetereka. Wale walio madarakani wana wajibu mkubwa kwa umma, na wasiwe chanzo cha ghasia kwani Mwenyezi Mungu Hapendi ghasia. Viongozi wa Kiislam wametakiwa kufuata mifano iliyopo. Hazrat Umar (r.a) alitawala vizuri kiasi hiki ya kwamba wakati wa utawala wa Wakristo wafuasi wa dini ya Kikristo waliomba urudi utawala wa Kiislamu. Kinachotakiwa ni taq'wa - ucha Mungu, jambo ambalo kwa bahati mbaya halipatikani miongoni mwa Waislam hivi leo, si watawala wala watawaliwa. Muongozo kamili kwa Waahmadiyya ni kujiepusha na ghasia hizi na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu, Mwenyezi Mungu siku moja Atasikia maombi yao. Na ikiwa viongozi wao ni waovu Mwenyezi Mungu Atawaepusha nao.

Mabadiliko hayo yanayofanyika yanaweza kuleta amani kwa muda mfupi na sio kwa kudumu. Madaraka yakipatikana kupitia uasi au mapinduzi baada ya muda utawala mbaya na wa mabavu hurejea tena. Kwa hiyo ombeni kuwa Mwenyezi Mungu Asiwapatie kiongozi katili. Mwenyezi Mungu Aufanye ulimwengu wa Kiislam uelewe haki zake na wajibu na haya ndiyo mafundisho safi ya Islam.

Mwisho

Jumuiya ya Burundi yazidi kuimarika

Na Ustadh Issa Ali Malenge
Bujumbura



Ustadh Issa Ali Malenge

Burundi ni nchi ndogo iliyopo kwenye ukanda wa maziwa makuu Barani Afrika. Kwa upande wa kaskazini nchi ya Burundi imepakana na Rwanda, kusini mashariki imepaka na Tanzania, na kwa upande wa magharibi imepakana na Jamhuri ya demokrasia ya Congo, pia upande huohuo wa magharibi imeungana na ziwa Tanganyika. Ingawa nchi ya Burundi ni ndogo lakini inaidadi kubwa ya watu, Inakadiriwa kuwa Burundi ina zaidi ya watu milioni nane. Idadi hiyo inaifanya nchi ya Burundi kuwa ya pili Barani Afrika kuwa na idadi kubwa ya watu ktk eneo dogo ikifuatiwa na Rwanda , Asilimia kubwa ya watu wa Burundi wanatoka katika kabila la Wahutu, pia wapo Watusi na Watwa , Haya ndio makabila ya wenyeji; pia wapo watu wengine wa makabila tofauti kutoka sehemu mbalimbali za dunia, Kwa upande wa dini asilimia kubwa ya watu wa Burundi ni wakristo wa madhehebu ya Katolic, Inakadiriwa kuwa asilimia 62 ya warundi ni Wakatolic, na asilimia zilizo salia ni Waislam, Walutheri, na wenye imani za kimila, Kwakuwa Burundi ina rasilimali chache zikilinganishwa na idadi ya watu waliopo, hali hiyo inaifanya nchi ya Burundi kuwa na idadi kubwa ya watu maskini, ikilinganishwa na nchi nyingine Barani Afrika.

Historia inaonyesha kuwa Burundi ilianza kuwa dola huru la kifalme tangu karne ya 16, Lakini mwaka 1903 nchi ya Burundi ilikuwa koloni la Ujerumani, Baada ya vita vya kwanza vya dunia Wajerumani waliachia koloni hilo, Hivyo likachukuliwa na Ubelgiji, Mwaka 1923, Ubelgiji ulililweka Taifa la Burundi chini ya utawala wake, Baada ya vita vya pili vya dunia, Umoja wa mataifa (UN) ulitangaza kuitambua Burundi kama koloni la Ubelgiji. Lugha inayozungumzwa nchini Burundi ni kirundi, kifaransa na kiswahili ktk baadhi ya maeneo. Mwaka 1962, Burundi ilijipatia uhuru wake kutoka kwa Ubelgiji, Baada ya uhuru, Burundi ilikumbwa na machafuko ya kugombea madaraka kati Watusi na Wahutu wenye msimamo mkali, machafuko hayo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe yalidumu kwa muda mrefu na athari za vita bado zipo mpaka leo, Ingawa vita vimekwisha. kwa sasa Burundi hakuna vita, maisha yanaendelea kama kawaida na kwa sababu ya amani iliyopo huenda maendeleo makubwa yakapatikana ktk siku za usoni, inshalla,

HALI YA JAMAAT AHMADIYYA NCHINI BURUNDI,

Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya nchini Burundi inajulikana kwa jina la COMMUNAUTE MUSULMANE AHMADIYYA DU BURUNDI , Waislam wa Ahmadiyya nchini Burundi walianza kupatikana mwishoni mwa miaka ya themanini, kupitia kwa Wanajumuiya waliofika Burundi kibiashara kutoka maeneo ya Tanzania, Kenya, na Uganda, Baada ya muda mrefu wanajumuiya wa Burundi waliendelea kuongezeka na kuimarika, pia walianza kusali sala za pamoja. Wakati wote huo walikuwa wakijiongoza wao wenyewe kutokana na elimu kidogo waliyopewa na wanajumuiya waliofika mara kwa mara nchini Burundi, pia walikuwa wakipata magazeti na vitabu mbalimbali kutoka Tanzania, Pia Jamaat ya Nchini Mauritus ilikuwa ikiwatumia jarida la LE MESSAGE,del Ahmadiyyat, jarida linaloandikwa kwa lugha ya kifaransa, ambalo hutoka kila mwezi . Vyote hivyo viliwasaidia sana ktk harakati zao za kueneza Jumuiyya nchini Burundi

Mwanzoni mwa miaka ya tisini mipango ya kuisajili Jumuiya ilianzishwa, kupitia Amir wa Jamaat ya Tanzania katiba ilitengenezwa, Lakini mipango yote ilivurugika kutokana na vita vilivyozuka mnamo mwaka wa 1994, kutokana na vita hivyo Wanajumuiya walisambaratika na mipango yote ilivurugika, Baada ya vita Wanajumuiyya walianza kujikusanya tena, hata hivyo wengi walibaki uhamishoni, Mwaka 1999 Jumuiyya ya Ahmadiyya ya Tanzania ilituma Mwalimu kwa ajili ya kushughulikia usajili, hata hivyo hatukufanikiwa kusajiliwa, mwaka 2001 harakati za kuisajili Jumuiyya zilianzishwa tena na kwa fadhili za Allah, mwezi novemba mwaka wa 2003 Jumuiya ya Burundi ilisajiliwa rasmi na serikali, Baada ya kupata usajili harakatia za Ahmadiyya ziliimarishwa, Tangu wakati huo Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania imekuwa ikituma walimu hapa Burundi kwa madhumuni hayo, pia baadhi ya vijana kutoka Burundi walipelekwa ktk chuo cha dini (JAMIA AHMADIYYA) kilichopo Morogoro kwa madhumuni ya kujifundisha dini ili waje kuimarisha Jamaat yetu ya Burundi. ifahamike kuwa Jumuiyya ya Burundi ipo chini ya usimmizi wa Jumuiyya ya Tanzania. Wanajumuiya wengi wanapatikana ktk jiji la Bujumbura ambao ndio mji mkuu wa Burundi. Ktk jiji hili kuna Jamaat tatu na sala ya ijumaa husaliwa ktk Jamaat ya Buyenzi. Buyenzi ndio eneo lenye Waislam wengi zaidi kuliko maeneo mengine hapa ktk jiji la Bujumbura, Wanajumuiya wengi pia wanaishi ktk mtaa huu, Hata Mwalimu pamoja na Rais wa Jamaat wanaishi Buyenzi. Pia wapo Wanajumuiyya wengine nnje ya Jiji la Bujumbura, Ktk Tarafa ya Nyanza-lac Mkoani Makamba wapo wanajumuiyya ambao wametoka Tanzania. Wanajumuiyya hawa walikuwa wanaishi Mkoani Tabora ktk kambi ya wakimbizi wa Burundi iliyopo Ulyankulu. Kwa sasa wamerejea nchini mwao na kwa pamoja tunashirikiana ktk harakati za kuendeleza Jumuiyya nchini Burundi. Hivi karibuni nilifungua rasmi kituo cha sala chenye vyumba viwili kimoja cha wanaume na kingine cha wanawake, Jengo hilo limejengwa na wanajumumuiyya wenyewe chini ya usimamizi wa Rais wa Jamaat ya Nyanza-lac ,mzee Saidi Mtuye.

Changamoto zinazo tukabili katika harakati zetu za kuiendeleza Jumuiyya ni nyingi. lakini kwa fadhili za Allah tunaendelea kupiga hatua. kwani mwenyezi mungu alikwisha mwahidi Hadhrat Mirza Ghulamu Ahmad kuwa ujumbe wako utaenea pembe zote za dunia,Pia mwenyezi mungu ameeleza ndani ya qur,an tukufu kuwa bila shaka mimi na mitume wangu ndio tutashinda (58:22) Mashekhe wamekuwa wakijaribu kuwa hofisha watu ili wasijiunge na jumuiya kwa kuwaambia kuwa Waahmadiyya si Waislam jambo ambalo ni uongo mtupu dhidi yetu, hata hivyo Mashekhe hawa wanatimiza bishara iliyo ndani ya qur,ani tukufu inayosema kuwa zama atakapo kuja Ahmad «ataitwa kwenye Islam» (61;7-8) Zama ambazo alitabiriwa kufika Ahmad ni zama ambazo uislam utakuwa umekwisha paa ktk nyota ya kilimia (bukhari kitaab tafsir) hakuna shaka kuwa zama hizo ndio hizi zama zetu ambazo mtume Muhammadi (s,a,w) amezitaja katika hadithi yake iliyopokelewa na Hadhrat Ali (r,a) inayosema kuwa» Ni karibu iwadie juu ya watu zama ambapo hakitabaki chochote cha Islam ispokua jina lake wala hakitabaki chochote cha qurani isipokuwa maandishi yake. (ktk zama hizo) misikiti yao itaendewa na watu wengi lakini itakuwa mitupu upande wa mwongozo ; Maulamaa wao watakuwa wabaya sana kuliko wowote walio chini ya mbingu, kutoka kwao fitina itatokea na itawarejelea wao wenyewe» (kanzul ummal) maelezo haya yanatuonyesha kuwa uislam wa kweli utafundishwa na Imam Mahdi (a,s) ambaye ni Sayidna Ahmad as. Mtume Muhammadi (s,a,w) akitoa maelezo juu yake anasema» Wakati Imam Mahdi aje mjiunge nae ingawa njia iwe ngumu (hata kwa kutambaa juu ya theluji) kwa maana yeye ni Mahdi -khalifa wa Mwenyezi Mungu, Basi msalimieni kwa kusema kwamba Ee hazina ya Elimu na jukwaa la utume, Salamu na amani kwako».(Biharul Anwar jl,13) Mashekhe ambao wanajiona wao wapo kwenye mwongozo wanajidanganya na hawana njia ispokuwa kujiunga na Jumuiyya hii ya mwenyezi mungu, Tumekua tukifanya Tabligh maeneo mbalimbali na watu wenye mioyo safi wamekuwa wakijiunga na jumuiyya.

Mipango yetu mikubwa ni kuendelea kuitangaza Islam chini ya bendera ya Hadhrat Ahmad (a,s) kama ilivyo fundishwa na Mtume Muhammadi (s,a,w) . Ingawa Ahmadiyya ina muda mrefu hapa Burundi lakini kutokana na vita hatukupata muda wa kuitangaza sana Jumuiyya , kwa sasa vita vimekwisha, na Jumuiyya inaendelea kuimarika, Tunawaomba ndugu zetu Waahmadiyya mtusaidie katika maombi ili Jamaat ya Ahmadiyya katika nchi ya Burundi iwe Jamaat kubwa kama zilivyo Jamaat nyingine duniani. Neno letu la mwisho ni sifa zote njema zinamuhusu mwenyezi mungu mola wa walimwengu.



Mwl. Hashim Rashid ametutoka

Mwandishi wetu



Mwl. Hashim Rashid

Kwa masikitiko makubwa tulipokea taarifa za kifo cha Mwalimu Hashim Rashid aliyekuwa tawi la Mmeda Mtwara. ***Inna Lillahi wainn aIlahi Rajiuun.***

Mwalimu Hashim alifariki tarehe 10 Mei na kuzikwa siku iliyofuata. Sababu ya ajali ya kifo chake ilielezwa kwamba ni kuanguka wakati akiwa uwanjani akicheza mpira na alipokimbizwa hospitali ya karibu mauti yakamkuta akiwa njiani.

Mwalimu Hashim alianza kazi ya ualimu wa Jumuiya mwaka 2010 baada ya kumaliza mafunzo ya muda mfupi katika chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro.

Awali Mwalimu Hashim Rashid aliwahi kujiunga na Jamia Ahmadiyya, lakini akaomba kukatisha masomo hayo ili aweze kuendelea na masomo ya sekondari kabla ya kuwa mwalimu wa Jamaat.

Jumuiya ilimkubalia ombi lake, lakini pamoja na juhudi kubwa aliyoifanya mwalimu alishindwa kumalizia masomo yake ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kufiwa na wazazi wake wote.

Baadae mwalimu aliomba akubaliwe kuwa mwalimu wa Jamaat na ndipo akapatiwa mafunzo ya muda mfupi ambayo yalimfanya aanze kazi hiyo.

Mwalimu Hashim alikuwa ni msomaji mahiri wa Qur'ani Tukufu na aliendelea kupangwa kusoma Qur'ani katika hafla kadhaa za Jamaat ikiwemo Jalsa Salana.

Mwalimu Hashim ameacha mke na mtoto mmoja.

Mwenyezi Mungu amuweka Mwalimu Hashim mahala pema Peponi, Amin.

Kenda mwalimu Hashimu,
Katuachia majonzi
Kwenda akiwa hirimu,
Kunazidisha simanzi
Mola Ampe maqamu
Kidumu chake kizazi
Allah Umwafu Hashimu,
Mjazi yako mapenzi

Historia kamili ya Mwl. hashim itatolewa toleo lijalo, Inshallah.

Bustani ya Washairi

TAREKHE YA AHMADIYYA TANZANIA

Kutoka toleo lililopita

799. Ya Mtwara haya hapa, Ni Nia yangu kuwapa,
sitathubutu kuchupa, Mtwara nikaachia.

800. Ni wajibu kuitaja, kwani zimumo faraja,
na hazina si iwaja, mwongozo kwa waelewa.

801. Ni khamsini na sita, huko nyuma tulopita,
bwana mmoja wamwita, ngoja nitakuambia.

802. M. Khamis Chilumba, ni mtembezi sambamba,
mtambuzi si mshamba, riziki hujitafutia.

803. Mwaka huo alifika, Rufiji kuangaika,
Mungu bariki Rabuka, kakumbana na Jamia.

804. Alijulishwa Jamia, Jamia Ahmadia,
Ifikile Tanzania, Yatakiwa kuijua.

805. Kila mtu atakiwa, vizuri kuielewa,
na bila ya kuchelewa, anapaswa kuingia.

806. Ujaji wa Masihia, hata kifo chake pia,
vitabu kufunguliwa, mwenyewe kujisomea.

807. Kasoma akatosheka, kabaki khofu na shaka,
akijiunga haraka, nini kitatokea?.

808. Rufiji akaondoka, na Mtwara akafika,
kamuona Mubaraka, mambo yakaendelea.

809. Maulana Mubaraka, kufahamui alitaka,
wapi palo tataniko, bado hajapaelewa.

810. Akaulizwa Chilumba, mbona mdomo kafumba,
hasemi wala kuomba, nini kimemtokea!

811. Chilumba akaeleza, mambo yalomshangaza,
khasa anapojilaza, kuna mtu humjia.

812. Ndoto inayo mjia, ni hii: akamwambia;
“kuna mtu unijia, usiku kijilalia.

813. Hufika mtu abidi (mja), Anaitwa Ahmadi,
hunihimiza zaidi, nyumbani mwake kwingia”

814. Ndoto inaashiria, watakiwa kuingia,
Jamii Ahmadia, Mubaraka kamwambia.

815. Si siku nyingi kupita, Chilumba hakuwa tata,
Baiati kakamata, Jumuiya kaingia.

816. Baada ya kujiunga, watu wakaja mzonga,
baadhi walimgonga, walihisi kapotea.

817. Kwa kuwa hawakupenda, walimfanyia inda,
kashifa na kumponda, hadi apate rejea.

818. Chilumba kasonga mbele, uimara vile vile,
wakakata tama wale, yeye akaendelea.

819. Mola kishaye alipe, kaje Mzee Mrope,
Bwana mitawa si lepe, wali ni nyuma vya pua.

820. Newala yapo matawi, mengi yaliyo stawi,
hayatishwi na uchawi, Allah wamtegemea.

821. Na habari za hakika, kutoka kwa muhusika,
ambazo nimezidaka, Mtwara yaendelea.

822. Kwa mkutano wa mwaka, wengi sana wanafika,
sijaona wamechoka, naona waendelea.

823. Ufunguwe masikio, ya watu tuwaitao,
tunaomba waje mbio, kufuata Jumuia.

824. Kajiunga Kasambula, na wengine kwa jumla,
baadaye si kwa hila, waila kwa kuelewa.

825. Si walala kipopopo, jamia Lulindi ipo,
Masasi Mjini ipo, motomoto Jumuia.

826. Tupe nguvu na uwezo, wewe ndiye wetu nguzo,
Bariki mazungumzo, yetu tunapoyatoa.

827. Hata kule Nachingwea, jamia imeenea,
kila unapoingia, Khabari utasikia.

828. Kwa michango na sadaka, wakulima wakumbuka,
wavuna watoa zaka, wala hawaja sinzia.

829. Ya Allah wape uwezo, zaidi kuliko mwanzo,
wengi tupate mafunzo, kwao na wengine pia.

830. Tuliza akili zao, wasikize tusemayo,
wajuwe mjumbe wao, wa zama alotokea.

831. Bada ya kutoka Mtwara, sasa nimeona bora,
kwa kupeana ishara, tuelekee Songea.

832. Ni hapa tumeshafika, wenyeji washughulika,
si kwa tabu na mashaka, bali kwa kilimo pia.

833. Mahindi walima sana, na tumbaku yalingana,
na kahawa yafatana, wala hawajaachia.

834. Maharage na mtesa, tena hulima kwa seso,
kwa kilimo cha kisasa, cha kutumia mbolea.

835. Wali wengi wapagani, na waenda kanisani,
waenda misikitini, wa haba tangu tangia.

836. Unaweza kuuliza, kama hali ndio viza,
nini kilichofanyika, kufika Ahmadia?

837. Ifatavyo nitajibu, nawe soma taratibu,
uimaizi sababu, jamia kuwa Songea.

838. Fadhilullahi Bashiri, alipo akihubiri,
kule Lindi kwa uzuri, wengi aliwavutia.

839. Kati ya walovutiwa, mmoja ni mzaliwa,
mzaliwa wa mkowa, wa Ruvuma wasikia.

840. Bwana huyo wa Songea, alijunga Jamia,
akiwa Lindi atua, mamboye kifatilia.

841. Ni Zuberi Abdullah, alofanya kila hila,
baada kula chakula, kingine alichukua.

842. Hicho alichochukua, alipeleka Songea,
hawapa kuangalia, kama kitasaidia.

843. Alikwenda kuonesha, pamoja kuwajulisha,
alonacho kwenye kasha, nduguze kapelekea.

844. Alipofika Songea, ujumge kawatolea,
nduguze kawaambia, kudhihiri Masihia.

845. Akawaamia: Matanga, na mchele wa mpunga,
kwa marehemu si kinga, bure wanawapikia

846. Hayo watu wamejaza, Mtume hakufanyiza,
manani hakuagiza, kwa uroho wametia.

847. Kawaambia wafahamu, sasa tunaye Imamu,
Sayidna muadhamu, Ahmad masihia.

848. Kinavyo eleza kisa, kaja badala ya Issa,
na kisa siyo mkasa, yabidi kufafanua.

849. Watu hawakuyaridhi, waila yaliwaudhi,
Zuberi alowaidhi, wapi aliko pokea.

850. Akawapatia jibu, yote ya kwenye vitabu,
Quruani mahabubu, na khadithi za Nabia.

851. Maneno ya Quruani, walionyeshwa bayani,
khadithi za vitabuni, walisomewa sawia.

852. Ndipo waliwaendea, Mashekhe wao kwambia,
khabari waloambiwa, wapate nao kujua.

853. Usemi walipokea, Mashekhe wakatongoa,
na wao wamesikia, hao watu wapotoa.

854. Hao ni Makadiani, waharibifu wa dini,
hawafai asilani, makafiri asilia.

855. Ali Saidi Amiri, Shekhe Hinduka Amir,
na mwingine mshauri, khabari walipokea.

856. Mwingine Shekhe Katobe, Khalfani ni mbabe,
akiamuru madebe, yapigwe kwa jumuia!

857. Si siraha madhubuti, khafifu ya hati hati,
walipoteza wakati, badala ya kuokoa.

858. Yao hayokusadifu, yetu yali matukufu,
waso na nafsi chafu, vyema waliangalia.

859. Walisoma Msahafu, wa tafsiri Tukufu,
na maelezo sufufu, kuhusu Ahmadia.

860. Yalikolea vichwani, waliacha upinzani,
wengine walisaini, baiati ya Jamia.

861. Wakajiunga Jamia, Ikachemka Songea,
si kwenda si kurejea, ni hayo ya kuongea.

862. Mlango waliogonga, walojitowa muhanga,
wa mwanzoni kujiunga, majina nawatajia.

863. Aliy Faraji Mbawala, Faraji Juma waswila,
wote wakaona, alla!, kwani wasiwe Jamia.

864. Na Abdallah Hanyanya, nduguye Isa Hanyanya,
juhudi waliifanya, wakawa Ahamdia.

865. Waliongeza uzito, kisha waliwasha moto,
upya na wenye fukuto, masuni walichukia.

866. Waliona kila leo, Ahmadiyya ni hao,
wazidi idadi yao, si kwamba inapungua.

867. Ikawa sasa nukusi, kaingia ibilisi,
wakafika mapolisi, mambo kuyaulizia.

868. Kwao lili la jabu, hawakujuwa sababu,
ipo sababu mujibu, wao hawakutambua.

869. Kukawa kule Likonde, nenda huendako wende,
Jumuiya kila pande, khabari zilienea.

870. Palikuwa Maulidi, ni pale pale biladi,
shekhe Hinduka kanadi, wapigwe Ahmadia.

871. Ahmadiyya khatari, kwa kweli sio wazuri,
dini wanaikhasiri, na watu wawapotoa.

872. Ni kauli ya masuni, ambayo wakibaini,
kuwambia wa mjini, kuhujumu Jumuia.

873. Zasemwa hizo khabari, mwalimu wetu Zuberi,
yu papo akibusuri, kupigwa kastukia.

874. Alipigwa kwa makonde, ili muradi aende,
bali palikuwa mbinde, vurugu ikatokea.

875. Alioneka Zuberi, kenda pale kwa ushari,
ikatolewa shauri, Zuberi kashtakiwa.

876. Zuberi kashtakiwa, hukumu ilitolewa,
alipe shilingi mia, faini aliyopewa.

877. Akishindwa penginepo, kutowa hayo malipo,
ende jela hapo hapo, bila ya kusubiria.

878. Sasa kwa miaka ile, shilingi mia segele,
kuzipata pesa zile, mambo yalokitatia.

879. Hakimu bwana Katepa, Bwana Zuberi kalipa,
na wala hakuzikopa, kwa mtu kuzichukua.

880. Ni khamsini na nane, bado mazuri mengine,
mia hizo wake wane, waweza kujiolea.

881. Zikapelekwa khabari, Dar kwa shekhe Amri,
Songea yalodhihiri, yote walimuambia.

882. Hakikishiwa Amri, ya kwamba hilo shauri,
hakuona kuwa zuri, atalishughulikia.

883. D. O. Kafanya kazi, kafanya upelelezi,
baada ya uchunguzi, khatuwa akachukua.

884. Alimuita Hinduka, Zuberi naye kafika,
Katepa kababaika, hukumu aliyotoa.

885. Bwana shauri kasema, huku Katepa kakwima,
mambo ya dini si vyema, mahakama kuingia.

886. Acheni mambo ya dini, yaishie vitabuni,
marufuku kortini, Katepa aliambiwa.

887. Ndipo katowa amri, kwa faini ya Zuberi,
arejeshewe dinari, zake alizozitoa.

888. Naam, kweli ni kweli, kamwe haiwi batwili,
kunako Jalali, ndiko anaegemea.

889. Wazushi hufa na feli, washindao ni wakweli,
mlijuwe jambo hili, si siri nawaambia.

890. Sisi tulisusuliwa, kwa mambo yaliyo sawa,
papo tunakufurishwa, kwa furaha ya mashia!

891. Tazameni mara tatu, uacheni utukutu,
dunia hino si kitu, watu watawakimbia.

892. Tumia akili yako, alokupa Mola wako,
mjuwe mjumbe wako, wa zama nakumbushia.

Endelea Uk. 7

Kutoka Uk. 6

893. Sasa tunao ulimbo, tumetega kila jimbo,
tumepanuliwa mambo, shughuli zaendelea.

894. Jumuiya i Liuli, Namtumbo kukamili,
Luwegu mambo makali, Mahengo yaendelea.

895. Jamia ipo Lusewa, Nahoro mechukuliwa,
Mhukuru sawasawa ipo huko Jumuia.

896. Hii ni kubwa hisani, kutoka Kwake Manani,
sisi tutasema nini? Twamshukuru Jalia.

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu,
S.L.P. 376, Dar es Salaam

DUNIANI HATUNAE BWANA ABDU NASIBU

1. Bwana Mudiri sahibu, khabari hizi zitwae
Na kasha uzikutubu, wengine wajisomee
Ndugu yetu mahababu, duniani hatunae
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

2. Japo kufa si ajabu, kifo kina karahe
Kinatowesha adabu, nidhamu iwapotee
Mkaona ni adhabu, mwenzetu atangulie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

3. Furaha ikaharibu, ikajaa huzunie
Huzuni huwa karibu, kila unasi alie
Mkumbukapo twayibu, ambayo akitendae
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

4. Ndicho kinachonisibu, kwa hivi leo mjue
Kwa al-akhi Nasibu, acheni nilie mie
Tumepokonywa dhahabu, hata na weye ulie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

5. Bwana Abdu Nasibu, Duniani hatunae
Amefariki muhibu, tulotukisema nae
Tukipanga taratibu, mwingine asipangua
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

6. Ai! leo ameghibu, kafa tumebaki sie
Na tuvisome vitabu, tuketi tufikirie

Maswali hayana jibu, basi Allah tumwachie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

7. Ali mkimya ajabu, kinywache asifungue
Bali mwepesi kujibu, kwaye amuulizae
Mzuwiaji ghadhabu, hasira isitokee
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

8. Mjao alijaribu, Mola Akukimbilie
Kiasi alijaribu, ni wachache mfanoe
Kama kafanya dhunubu, naomba mghufirie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

9. Ya Rabi mpe Nasibu, msimamo apumue
Mpangie taratibu, wala usimuumbue
Mhesabie hesabu, nyepesi ajisikie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

10. Muache simuadhibu, bali umbarikie
Halafu umtanibu, na nari umuokoe
Umuepushe taabu, kwenye Janati mtie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

11. Ewe Jalalu Wahabu, tafadhali nisikie
Mlipe nyingi thawabu, motoni asiingie
Umpe pepo nasibu, ende huko atulie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

12. Pole kizuka akabu, lia na uvumilie
Sote tu wafu awabu, nani hapa abakie
Tumuombee Nasibu, peponi akatulie
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

13. Nanyi wana ni wajibu, mama mumsaidie
Kila njia mjaribu, kwa karibu kuwa nae
Simbebeshe harubu, ya nyuma akumbukie.
Duniani hatunae, Bwana Abdu Nasibu

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu,
S.L.P. 376, Dar es Salaam

KATWEKA BIN NASIBU, ULIMWENGUNI HAYUPO

1. Mhariri hili shika, na tafadhali pokea
Kwenye gazeti andika, haya yaliyotukia
Mmoja wetu katoka, ameiaga dunia
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

2. Ndugu aliyetutoka, isimu tawatajia
Ni mshairi wa shoka, (Jicho) alijipangia
Abdu Nasibu kaka, jina la kutangulia
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

3. Mwezi wa Mei mwishoni, msiba umetokea
Kafa hospitalini, alikokiugulia
Ni Muhimbili wodini, ndimo alimojifia
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

4. Khabari zikasikika, kutoka kwa Jumuia
Nasibu ametutoka, maziko twatazamia
Kesho kipenda Rabuka, yote yatafatiliwa
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

5. Juni mosi ikafika, saa nane kutimia
Mazishi yalifanyika, kule tunakozikia
Watu wengi walifika, maziko kuhudhuria
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

6. Na swalatu janaiza, Amiri wa Jumuia
Ndiye aliyeongoza na dua kumuombea
Kasha Ame alikoza, machache alitongoa
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

7. Mwalimu Ame lisema, kwa upande wa Jamia
Hadi hapo wamekoma, hakuna cha kuzidia
Akawashukuru uma, wote walohudhuria
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

8. Karamu na mahitima, talakini twaachia
Si mafundisho salama, Rasuli hakutwambia
Kuyafanya sio vema, madhambini twajitia
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

9. Katika maziko yake, ndiyo yaliyotokea
Ndugu na jamaa zake, wa damu wakasikia
Moyoni mwako yaweke , khatima utatumia
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

10. Labda tuwadhukuri, nyuma wanofatilia
Wako nasi kwa khabari, hizi twazisimulia
Wazikariri vizuri, mengi wapate kujua
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

11. Historia yasema, Babaye alichukia
Abdu aliposema, ajiunga Jumuia
Alimwambia kuhama, alihisi kapotea
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

12. Abdu alisimama, imara kiomba dua
Mwenyezi Mungu Karima, hali ya shida kutoa
Zikazamishwa hasama, salama kachipua
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

13. Sisi wana Magomeni, wa tawi la Jumuia
Sana tunayo huzuni, twasikitika twalia
Bali tutafanya nini, Allah analoamua
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

14. Ali kiongozi wetu, akituongoza njia
Kipita kwenye misitu, ilotata kutatia
Akiwa kama mwenzetu, Nasibu alitatua
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

15. Tumekuwa naye siis, kwa miaka kupitia
Pamoja tukijilisi, swala tukijiswalia
Michango tena kwa kasi, kituhimiza kutoa
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

16. Ali muhubiri mwema, wasuni wamatambua
Mikumi pale kivuma, alijulika Jamia
Masheikh na maamuma, wakikwepa kumwendea
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

17. Ya Ilahi Mola wetu, Nasibu katangulia
Twaomba Muumba wetu, mpokee kwa huria
Muweke kwenye Janatu, aliko kitegemea.
Katweka bin Nasibu, ulimwenguni hayupo.

Jamil N. Mbambwa
Kwa niaba ya tawi la Magomeni Kagera
S.L.P. 376
Dar es Salaam

Mzee Nasibu katutoka

Kutoka Uk. 2

mfanyakazi wa Wizara ya Elimu. Yeye alipojiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya, baba yake, mmoja wa wazee awatan na wasomi katika jiji la Dar es Salaamalimtenga na kumfukuza nyumbani kwake. Mateso aliyoyapata yalikuwa makubwa na kaambiwa atoke katika nyumba aliyokuwa anakaa. Aliondoka na katu hakutetereka na sheikh Muhammad Munawwar alizidi kumuimarisha na akaimarika kweli.

Kitu kikubwa kilichomsaidia ni usomaji wa vitabu vya Jumuiya. Enzi hizo vitabu vya Jumuiya hususan katika Kiingereza vilikuwa bwerere visivyokuwa na msomaji. Wasomi wa wakati huo akiwemo bw. Nasibu walipewa vitabu vingi vya Kiingereza ambavyo vilizidi kuwaimarisha.

Mivutano mingi ilifanywa na baba yake bwana Nasibu ili atoke katika "Ukadiani" lakini bwana Nasibu alionesha uimara na uvumilivu wa hali ya juu.
Kwa khulka bwana Nasibu alikuwa mpole, asiyependa shari wala kelele, lakini lilipokuja swala la kutetea imani yake alisimama kidete na kutetea imani yake.
Kutokana na mapenzi ya Jumuiya alipostaafu alikuwa anafanya kazi yakujitolea msikitini kwa kuchapa barua na kazi nyingine alizopewa. Kwa sababu ya uhodari wake alipewa kazi nzito ya kuwa Mhariri wa Mapenzi ya Mungu. Jambo moja lililonofurahisha ni kwamba mara alipoteuliwa alijiandikisha na chuo fulani ili ajifunze uandishi wa habari. Mafunzo hayo aliendelea nayo kwa muda. Pia aliniomba nimtafutia mtu aliyebobea katika uandishi wa habari ili aweze kumfunza. Tulibahatika kumpata bwana Ndimara Tegambwage, mwandishi mwenye jina na mshairi wa gazeti la Mwanahalisi ambaye alimpa maelezo mengi.

Toka miaka mingi bwana Nasibu Hija alikuwa mshairi na alihusika katika kuandikisha chama cha washairi kilichoundwa mwaka 1958. Kuhusu lugha ya Kiswahili, umahiri wake alikuwa mkubwa na sisis tunaotoka bara hatukukosa cha kujifunza kutoka kwa mzawa huyu wa Mzizima.

Bwana Nasibu alikuwa ni mtu wa msimamo, akisha

shika kitu chake vigumu kumtikisa. Nakumbuka ziliztoka lawama za utumiaji wa baadhi ya maneno ambayo ni aibu kidogo kuyatamka, yeye alisema tutayandika hivyo hivyo kwani ndivyo yanavyofahamika katika lugha ya Kiswahili.

Akiwa Mhariri wa Gazeti la Mapenzi ya Mungu alikuwa nashauriana na waandishi wake na hata kuwapa fursa ya kuandika tahariri. Vitu vinavyohusiana na utafiti alivipenda sana na aliwahimiza waandishi waandike juu ya mambo hayo ya utafiti.

Vitabu, kama nilivyokwishasema vilikuwa vilikuwa kivutio kikubwa sana kwake. Nakumbuka maonesho ya vitabu yalifanyika makumbusho mtaa wa Shaaban Robert, alinishairi twende na tukaenda na huko tulipita katika vibanda vingi na tukapata vitabu viwili vilivyogusa Ahmadiyya kwa njia moja au nyingine. Vitabu hivyo ni Qadianism, The Crescent and the Cross. Kila alipopata kitabu au makala inayoshambulia Ahmadiyya alihakikisha masahihisho yamefanywa na ukweli umewekwa bayana.

Bwana Abdulrahimu Nasibu Hija alipata fursa nzuri ya kuitumikia Jamaat, fursa ambayo wengi hawaapti. Aliwahi kuwa mjumbe wa Majlis Amila, akiongoza idara ya Uchapishaji na aliwahi kuwa Rais wa tawi la Magomeni Mikumi. Ushiriki wake katika shughuli za Jumuiya ulikuwa ni wa hali ya juu, sikumbuki kuikosa Jalsa Salana hata moja. Ni ufaulu ulioje kuondokla katika dunia hii wakati ukiwa na imani thabiti. Mwenyezi Mungu ampokelee juhudi alizofanya katika kuitumika Jamaat Ahmadiyya – Uislamu wa kweli.

Majonzi thama mapenzi, katuondoka Nasibu
Hija ni wetu Kipenzi, kwetu ali ni sahibu
Roho zimepata ganzi, kuondoka mahababu
Rabi maskani, pale palipoinuka

Ni mshairi wa tenzi, tungo zilizo twaibu
Za kusifu mwenye Enzi, Yailahi ya Wahabu
Tungo zake ni kurunzi, za mwanga wenye kutibu
Rabi maskani, pale palipoinuka

Jicho si jicho la panzi, ali jicho la aibu
Kila walipo washenzi, watu waso na adabu
Mara huwapiga konzi, ili wawe waraibu
Rabi maskani, pale palipoinuka

Na gazeti la Mapenzi, alichonga yake nibu
Akawa yeye mlinzi, tena mzlinzi shababu
Na ule wake ujuzi, ukavuta wa karibu
Rabi maskani, pale palipoinuka

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

UGONJWA

Wakati alipokuwa akitoa hotuba ya Ijumaa, terehe 18 Novemba 1910, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaeleza hisia zake kama yafuatavyo:

"Napenda sana nione kwamba Jumuiya hii inampenda sana Mungu na kumtii Mjumbe wake na kufahamu Kurani. Mola wangu pasipo kunitia katika majaribio na bila mimi kumwomba Amenijaalia fadhili zake nyingi tena kubwa. Yeye amenitimizia haja zangu sikuzote. Yeye Mwenyewe Ananilisha na kunivisha na kunipatia faraja. Amenijaalia nyumba, mke, watoto na marafiki wanyofu na wa kweli. Amenipatia idadi kubwa ajabu ya vitabu, na Amenipa nafasi ya kuvisoma na Amenijaalia afya njema, ujuzi na kila kitu kilichohitajika. Sasa mapenzi yangu ni – nami natumai kabisa kwamba Mola wangu Ananitimizia haja hii yangu pia – kwamba miongoni mwenu wapatikane wanaompenda Mungu na neno la Mungu Alilomteremshia Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, na kumtii Mungu, na kumfuata barabara Khatamun Nabiyyin wake. Huenda miongoni mwenu wapo wanaofuata Kurani Tukufu na suna ya Mtume Mtukufu s.a.w. Naomba kwamba nikiaga dunia hii, macho yangu na moyo wangu vitulie kuwahusu nyinyi. Sitaki kwenu ujira, wala sihitaji mnitolee kitu. Sitaki hata mmoja wenu aniamkie. Yote ninayohitaji ni kwamba muwe mnamtii Mungu, na mkiwa wafuasi wa kweli na Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, mzifikishie sehemu zote za dunia, kwa amani na urafiki, ujumbe huu: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu."

Baada ya sala akaamua kumtembelea Nawab Muhammad Ali Khan aliyerejea Qadian siku moja kabla kutoka Malir Kotla. Kwa kuwa ilikuwa safari ya maili moja na nusu takriban, akaamua kumpanda farasi jike, mnyama mwenye nguvu ambaye mtu fulani alimpatia zawadi mwanaye mkubwa, Abdul Hai, kijana mwenye umri wa miaka kumi na mmoja. Alipokwisha msogelea na kumpanda, mtu mmoja aliyekuwa amesimama hapo akaona vikuku viko juu zaidi na akajitolea kuvishusha kidogo chini ili aweze kupanda kwa urahisi, lakini akamkataza akisema kwamba vimewekwa hivyo kuwafaa watoto kwa hiyo visishushwe chini. Akapanda na kuondoka. Wale waliomwona akipita huku akiwa amepanda wakaona kwamba ingawaje farasi alikuwa anakwenda kasi, lakini yeye alikaa vizuri na imara na kufurahia kwenda juu ya farasi. Alipoingia mjini akalazimika kupitia njia nyembamba. Mahali fulani katika njia hiyo nyembamba farasi akaruka upande ghafla, akarushwa kulia, mguu wake wa kushoto ukanasa katika kikuku, na akatupwa upande wa kuume juu ya mwamba mmoja uliobenuka. Akapata vijeraha vidogo vidogo vingi na jeraha moja baya kwenye panja la kuume lililotoka damu nyingi sana. Alipong'amua kilichofanyika akasema kwa sauti ya juu: "Aliyetumwa na Mungu amethibitika kuwa mkweli." Hayo ndiyo marejeo kwenye ruya moja ya Masihi Aliyeahidiwa ambamo alimwona Maulawii Nuruddin ameanguka kutoka kwenye farasi. Alipoota ruya hii, hata Ahmadiyya mmoja katika Qadian hakuwa na farasi wa kupandika. Pengine funuo zake mbili zinataja tukio hilo. Mmoja ni: Uhai wa pili; na mwingine ni: Uhai uliotanguka.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa mtulivu kabisa, hakuhangaika hata kidogo. Msaada wa kwanza ukapatikana haraka na jeraha la panja likashonwa bila nusukaputi. Waliomtibu hawakuona mshtuko wa msuli mmoja waliposhughulikia kumtibu. Habari ya ajali ilipoenea wanaume kwa wanawake wakaelekea nyumbani kwake wakihangaika kuhakikisha wenyewe usalama wake. Kwa wanaume akasema atawaombea. Kwa wakina mama akapeleka ujumbe kwamba yeye hajambo, hana wasiwasi wala hofu; wapaswa kurejea nyumbani kwao wakiacha majina yao, naye atawaombea. Kuhusu shauri ya kwamba daktari mkuu wa Delhi anaweza kuitwa, akajibu: "Mtegemeeni Mungu. Tegemeo langu si madaktari wala matabibu. Namtegemea Mungu kikamilifu, nanyi mwapaswa kufanya hivyo."

Jeraha la panja lake likawa donda la kudumu na ugonjwa wake uliendelea kwa miezi mingi. Ilikuwa tarehe 19 Mei 1911, miezi sita kamili baada ya ajali, ambapo akaweza kwenda mskitini na kusalisha sala ya Ijumaa lakini hiyo ilikuwa kwa taabu. Hata hivyo katika kipindi kirefu cha kupata ahueni akajishughulisha kikamilifu na



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

kuweka mfano bora sana wa kujitolea kwa kutimiza wajibu.

Tarehe 29 Novemba 1910, akachapisha na kueneza ujumbe wake ambamo alisema:

"Jaribio ninamopitia ndiyo nafasi ya onyesho la jiha mbalimbali za huruma, rehema na fadhili za Mungu. Mungu Mtukufu Amenidhihirishia kujitolea kwa nyoyo za wengi ambao napaswa kuwa na upendo kwao. Wapo wengine ambao kuwahusu hao sikuwa na habari kwamba wanipenda mimi na wanajumuiya wenzao. Namna walivyonitumikia mchana na usiku katika siku za mimi kuugua huonyesha kiwango cha upendo wao, na ndiyo kwa njia hiyo Mungu Amedhihirisha sifa zao bora. Hiyo yahakikisha jinsi Mungu Anavyonitunza. Nawashukuru sana wote walioonyesha kwangu moyo mpole katika hali yangu hii ya hivi sasa.

Moyo wangu watulia. Hakuna ninayempenda zaidi kuliko Mungu, wala hakuna aliye msaidizi wangu na tegemeo langu jinsi Alivyo Yeye. Alinijalia fadhili zake na ukarimu wake bila hesabu katika hali yangu hii. Akanipatia kutoka huko asikoweza kuwaza yeyote. Ameondolea mbali hata njia dhahiri ya riziki yangu ambayo ndiyo kazi yangu ya utabibu na Ameniruzuku kwa njia za siri. Sidaiwi na yeyote kwa riziki hiyo iliyofika nyumbani kwangu siku hizi: Nawiwa na Mungu tu kwa hiyo yote. Hayo yote ni ajabu sana machoni mwa waonao."

Mnamo Desemba 1910, akatamka siku moja:

"Ugonjwa ni jaribio kwa njia nyingi. Matumizi yanapanda, na mapato yanapungua, na mtu huwa anawategemea wengine. Njia dhahiri ya kupata riziki yangu ilikuwa utabibu, ambayo imetanguka kwa sababu ya ugonjwa wangu. Wasiojua kweli hasa ya mambo yangu wakafikiri kwamba utabibu wangu ulikuwa ni njia ya kutimiza mahitaji yangu, na Mungu Ameiondoa sasa. Mke wangu akaniambia leo kwamba hana hela iliyobaki, na akasema: Hukufikiria katu kuugua. Katika hali ya ugonjwa mtu anaweza kukosa hata mahitaji la lazima ya maisha. Nikamwambia kwamba njia ya Mungu wangu kunihusu mimi si hivyo. Ningeliweka fedha akiba kama nisingelimtegemea Mungu kikamilifu."

Ikawa hivi kwamba pasipo kujua yeye, hawala mbili za posta zenye thamani ya rupia mia moja ishirini na tano zikawasili ili zilipwe kwake. Alipoarifiwa kuhusu hizo akajawa na maono mazito na akamsifu Mungu kwa moyo wote na akanena: "Ndivyo ilivyo fadhili ya Mungu wangu Mweza. Ameonyesha kwamba ananipatia pasipo kuhesabia ufundi wangu nikiwa tabibu, namna ambavyo haieleweki. Mke wangu hawezi kuitambua kwa sababu ya udhaifu wake. Imani yangu ni imara. Mungu wangu daima Ananitendea hivyo."

Maonyesho hayo ya Mungu kuruzuku yakaendelea sikuzote. Siku moja alimwagiza Sheikh Muhammad Taimur kutengeneza hesabu ya matumizi yote yaliyofanyika katika siku za maradhi yake kama vile dawa, bendeji na kadhalika, na fedha zote kwa jumla zilipwe kutoka katika fedha zilizokwisha patikana sasa. Akasema: "Mola wangu Aniruzuku. Sipendi kuwiwa na yeyote awaye. Yeye Ameniahidi kwamba Atanitimizia mahitaji yangu yote.»

Tarehe 15 Desemba 1910, taarifa ikatolewa kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. afya yake inazidi kuwa nzuri. Hana homa, wala hana kikohozi. Alikuwa bado dhaifu sana, ijapokuwa alipata nguvu kidogo. Vijeraha vyake viliendelea kupona pole pole, kimoja cha mdomoni kikapona kabisa na akawa hana shida kula na kuzungumza. Mara moja moja aliona shida ya kupata usingizi. Kila siku akasomewa Kurani Tukufu, asubuhi na jioni. Akaeleza maoni yake kuhusu baadhi ya mambo fulani na akatoa nasaha. Mzungu mmoja akaja kwa kumjulia hali, na Khalifatul Masihi r.a. akaongea naye kiasi fulani kuhusu Islamu.

Mkutano wa Mwaka ulifanyika tarehe 25, 26, na 27 Desemba 1910. Hadhrat Khalifatul Masihi akauhutubia Mkutano jioni ya Desemba 25 juu ya: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; na tena tarehe 27 Desemba, saa za jioni kuhusu: Silaha ya Dua. Akitoa hotuba yake ya pili alisema:

"Niombeni, nitawajibuni (40:61) ndiyo silaha moja, nayo yafaa sana. Pengine anayeitumia ni dhaifu na anaikataa faida yake. Ndiyo silaha ya dua ambayo imetupiliwa mbali siku hizi na wanadamu. Wanajumuiya wa Jumuiya yetu wanapaswa kuinoa na kuitumia. Wanapaswa kufululiza kuomba pasipo kuchoka kufanya maombi. Mimi naugua sana, wala hakuna awezaye kujua nitaishi muda gani; hivyo, nasaha yangu ya mwisho ni: Pamoja na 'Hakuna apasaye kuabudiwa ila Mungu', inoeni silaha ya dua. Kusiwe na farakano katika Jumuiya, kwani farakano likipatikana Jumuiya huadhibiwa na Mungu; kama ilivyosemwa ndani ya Kurani Tukufu: Basi waliposahau waliyoyakumbushwa, Tukawaokoa wale waliokuwa wakikataza maovu, na tukawakamata wale waliodhulumu kwa adhabu mbaya kwa sababu walikuwa wakiasi (7:166). Hadi sasa mlihifadhiwa msipatwe na adhabu hiyo. Hata maombi hayasaidii bila ya rehema na huruma ya Mungu. Kwa hiyo, nawasihini: Ombeni mfululizo; nakariri: Ombeni mfululizo ya kwamba Jumuiya ilindwe isipate kufarakana. Fadhili ya Mungu iliyojaaliwa Jumuiya mpaka sasa ni kwa sababu ya maombi. Niombeeni pia kwamba wasaidizi wangu wawe waaminio wanyofu, watiifu kwa Mungu, wema na wakarimu, wasioniasi. Nijaaliwe wabashiri ambao wakiwa na imani inayoeleweka akilini, watambue ukweli, wasiwe na tabia ya kupenda anasa za dunia, na zaidi ya kuwa wanyofu wafahamu suna ya Mtume Mtukufu s.a.w."

Akamalizia:

"Mwawiwa nami wajibu kadhaa:

1. Mmefanya baiati yangu na mnawiwa nami utii. Yule anayevunja ahadi atakuwa mnafiki. Nachelea isije yeyote akawa mnafiki kwa kuniasi.
2. Naomba kwa uchungu kwa niaba yenu.
3. Kwa sababu ya maradhi siwezi kufanya sujuda katika sala, hata hivyo nimewaombeeni kirefu na kwa bidii katika hali ya sujuda.

Basi kwa kukiri wajibu wenu kunihusu mimi, yawapaseni kuepukana na hitilafu na mifarakano."

Mkutano wa Mwaka ulipomalizika, akawaita Maraisi na viongozi wa matawi na akawaambia:

"Nimewaiteni kwani niliudhika kwa sababu hamkuonana nami

Endelea Uk. 9

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Kutoka Uk. 8

mwaka jana, nami nilikusudia ya kwamba nikibaki hai nitawatoleeni nasaha mwaka huu. Mimi hata sikupata kuwaza kwamba nitakuwa Kiongozi wa kirorho wa Jumuiya, lakini Mungu Alipotaka Akanifanya mara moja. Nyinyi ni viongozi katika Jumuiya, na bila shaka mara nyingi mwazikabili shida. Mtu anaweza kufikiri kwa nini yeye hakufanywa kiongozi na akaingiwa na chuki moyoni. Hali yangu mimi binafsi ni kwamba kama baada ya kufariki Masihi Aliyeahidiwa a.s., bintiye Amatul Hafidh aliye mtoto mchanga angelichaguliwa kuwa Khalifa, ningelikuwa wa kwanza kufanya baiati kwake, na kumtii jinsi nilivyokuwa namtii babake, nikiwa na yakini kwamba ahadi za Mungu zitatimia kwa njia yake pia. Kusudio langu kwa kusema hivyo ni kwamba mtu asiingiwe na tamaa kama hizo.

Nasaha yangu ya kwanza ni hii – nami nawaombeni kuiweka sana moyoni – kwamba mkikabili mishikili, zingatieni maagizo ya Mungu! Jiepusheni na mafarakano isije mkakwaa na nguvu yenu ikawatoka. Kaeni imara; bila shaka Mungu Yu pamoja na wakaao imara (8:47). Mungu Akiwa Mwumbaji wa tabia ya sili ya mtu, akatambua kwamba kutakuwa na mafarakano; basi akaagiza: Muwe imara; Mungu Yu pamoja na walio imara. Basi mkihitilafiana na kiongozi mmojawapo, kaeni imara. Mungu Atakuwa pamoja na yule akaaye imara kwa ajili ya radhi Yake.

Ninayo haki ya kuwasihini. Baada ya nyinyi kwisha kufunga ahadi kwamba mtanitii katika mambo yote mema, nawaambieni kunitii katika jambo hili: Jiepusheni na mafarakano. Wakati wowote mkikabili mafarakano, angukeni katika sujuda mbele ya Mungu ili mjaaliwe uimara. Msiogope mishkili; katika kila hali mtu hulazimika kuikabili. Mimi nalipata kuikabili ile yangu. Baadhi ya wanajumuiya wakaangukia kosa na wakafanya hatia ya ujuvi mkubwa na kukosa adabu; lakini nikavumilia. Hawakutambua walikuwa na wajibu gani kumhusu Kiongozi wa Jumuiya. Kutokutambua huo ni kwa sababu ya kukosa ujuzi. Lakini Mungu Alikuwa mwenye huruma; Yeye Mwenyewe Akanyosha nyoyo zao. Nyoyo zimo mikononi mwa Mungu na Yeye Akazielekeza zote hizo kwangu mimi, kwa hiyo hao na sisi na Jumuiya tutashuhudia huruma yake na ukarimu wake. Basi epukaneni na mafarakano nyinyi wenyewe na waelekezeni wanajumuiya wengine wayaepuke. Mungu Mtukufu Ameamuru kukaa imara katika hali kama hizo.

Jambo jingine ninalotaka mlizingatie ni kwamba katika baadhi ya sehemu ambapo kuna wanajumuiya wengi, maendeleo zaidi yamekuwa kidogo. Naelewa sababu yake, na ninawasihini kujaribia dawa mbili. Ya kwanza ni kwamba viongozi wamwombe Mungu kwa uchungu. Mwaju a kwamba jua au mwezi unapopatwa, sala inasaliwa. Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa akihangaika sana wakati wa jua na mwezi kupatwa, ingawaje alielewa hilo huwa sawa na kanuni ya asili inayofanya kazi ulimwenguni, kama ilivyosema Kurani Tukufu: Na mwezi Tumeupimia vituo (36:40). Alijua ya kwamba wakati wa kupatwa mwanga wa jua au mwezi haupungui, bali hukingwa usifikie ardhi. Hata hivyo alikuwa anafadhaika, kwani aliagizwa kufikisha ujumbe na akahofia isije kikwazo fulani kikaja kati kuzuia ufikishaji wa ujumbe wake. Kwa hiyo wakati wa kupatwa jua au mwezi akafanya maombi, akatoa sadaka, akatoa dhabihu na akawapa uhuru watumwa.

Wataalamu wajinga wa falsafa wakasindwa kutambua siri hii, lakini Nabii anatambua kwamba yeye mwenyewe anang'ara, hata hivyo anachelea isije mng'ao wake ukazuilika jinsi nuru ya jua au mwezi inavyozuilika wakati wa kupatwa. Basi anamwomba Mungu na kutoa sadaka. Kutoa sadaka ni dawa ya pili kwa kuondolea mbali kizingiti cha kati katika maendeleo. Zingatieni sana kwamba popote maendeleo yakipungua, viongozi wa hapo wapaswa kutawadha na kufanya maombi ndani ya sala na kutoa sadaka binafsi ili Mungu Aridhike na kuondoa kizuizi katika njia ya maendeleo. Nawaamuruni kutoa sadaka, kwani sadaka na kutoa mali kwa wanaostahili huzima moto wa ghadhabu ya Mungu.

Mwishoni napenda kuwaonya kudhania viovu kuhusu utumiaji wa fedha za Jumuiya. Wahusikao na jambo hilo waliopo hapa katika makao mkuu ni waaminifu na wenye kutegemewa. Kwa hiyo msiwe na hofu kuhusu habari hii. Mimi nami ni mdhamini wa chochote ninacholetewa. Nataka kuwahakikishieni kwamba Mungu Hakunifanya mwenye tamaa ya mali. Sina tamaa ya mali. Nampa mke wangu fedha kiasi fulani maalum. Wala sina tamaa ya ukuu.

Nasogelea mwisho wangu. Mimi ni mpenda heri kwenu mwaminifu.



Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a., mwandishi wa kitabu hiki

Nawaombeeni daima dumu. Sikupokea fedha kutoka kwa baba yangu; lakini Mola wangu Amenipa sana na bado Anaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, tupilieni mbali dhana mbaya kuhusu habari hii. Stawisheni huba baina yenu, epukaneni na fitina, msimdhanie vibaya yeyote; mtu akiwakasirikieni muwe imara, na dumuni katika maombi.

Hayo yote nilikuwa nayo moyoni tangu mwaka mzima kwamba nitawaambieni. Baadhi yenu pengine walidhani kwamba nilikuwa na madhumuni ya binafsi katika kuwatakeni mnione. Sihitaji chochote kwenu. Jina langu huko mbinguni ni Abdul Basit, maana yake ni mtumishi wa Mpaji sana. Amenipa kila kitu kinachohitajika. Ni kubwa sana hisani yake juu yangu. Kitambo kidogo kimepita nilipoanguka kutoka juu ya farasi jike niliyekuwa nimempanda. Kama angalinipiga teke jichoni, ingelikuwaje hali yangu? Lakini nikalindwa kwa hisani Yake. Makosa mengi yalifanyika katika mwaka unaokaribia kwisha, lakini natumai kwa fadhili Zake kwamba makosa yote hayo hayatarudiwa katika mwaka unaokarubia kuanza."

Taarifa ya daktari ya tarehe 5 Januari 1911 ikaeleza ya kwamba vijeraha vya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. vilitibiwa kila siku katika siku za Mkutano wa Mwaka na akafungwa bendeji moja, lakini sasa majeraha yamepona na bendeji imeondolewa. Kwa sababu ya shughuli nyingi katika siku za Mkutano wa Mwaka na kupokea wageni na kuongea nao akapatwa na uchovu mwingi. Meno yake mawili yaliyomsumbua yakang'olewa. Akapatwa na homa kwa siku mbili. Sasa hajambo, lakini anapata maumivu ya neva mara kwa mara. Yu mchangamfu saa zote, hana shida au wasiwasi. Baada ya meno yake kuong'olewa akasema: "Kila maumivu yana malipo yake. Sasa naweza kunywa na kuyafurahia maji baridi."

Baada ya wiki moja ikaripotiwa ya kwamba bado anasumbuka kwa maumivu ya neva mara kwa mara na ana uvimbe shavuni unaouma ambao umesababishwa na meno yake kung'olewa.

Taarifa ya tarehe 19 January ikaonyesha kwamba maumivu ya neva yanaendelea mara moja moja, hana utulivu, usiku mmoja hakupata usingizi.

Dkt. Mirza Yakub Beig alitoa taarifa tarehe 22 Januari kuhusu maendeleo mazuri kwa kila jinsi. Mgonjwa mtukufu alilala vizuri usiku, hana homa. Anaendelea kupata nguvu kidogo kidogo. Daktari alipokuwa anatoka baada ya kumchunguza akamwuliza mgonjwa kuhusu chochote apendacho. Akajibu:

"Yote unayopenda moyo wangu ni kwamba Mungu Aniwie radhi. (Akarudia haya mara tatu) Napenda mwendelee kuwa watii wala msifarakane. Msilete ukinzani. Nimekwisha pata shibe ya dunia. Sina hamu ya kidunia. Kila nipendacho ni kwamba nitakapokufa Mungu Awe Amekwisha niridhia. Mwambie hayo kila mmoja. Siijali dunia hii. Nilijaaliwa nyingi na nilipewa nyingi, nilitumia nyingi na nilitoa nyingi. Sina tamanio tena. Wakati mwingine natamani nipate afya isije ugonjwa unaofululiza ukaharibu imani yangu. Mungu, nakuomba, niwie radhi.

Napenda sana kwamba kusizuke fitina katika Jumuiya yangu. Dunia haina maana kwangu. Nitaridhika sana kama mtaendelea na umoja. Siwezi kufanya sujuda kwa sababu ya ugonjwa wangu; hata hivyo nawaombeeni nikisujudu. Nimewaombeeni mara kwa mara kwa wema wenu. Sihitaji kwenu chochote, wala sina tamaa yoyote ya kidunia. Mola wangu Ananipatia kwa wingi kwa njia za siri, kwa wingi zaidi kuliko mahitaji yangu. Jihadharini na hitilafu na ukinzani. Mkiepukana na hayo mtabarikiwa sana na Mungu, na heshima yenu na nguvu yengu itadumu; la sivyo matapoteza kila kitu.

Mimi sikutoa agizo lotole kwa matilaba ya ubinafsi; maagizo yangu yote ni kwa kutafuta radhi ya Mungu. Tieni bidii katika kusali na kuomba kwa kudumu. Sala ndiyo dua. Msizidishe hitilafu na ukinzani; hivyo vimeleta uharibifu sana. Hitilafu zikizuka, kaeni kimya. Jiombeeni nyinyi na wapinzani wenu. Tubuni sana: Hamna mwabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad ni Mjumbe wa Mungu. Shikamaneni na Kurani. Isomeni sana na tendeni sawa nayo. Ama kunihusu mimi, namridhia Mungu kuwa Mola, Islam kuwa dini na Muhammad s.a.w. kuwa Mjumbe. Kwa hayo nawawekeni chini ya himaya ya Mungu."

Taarifa za baadaye za kidaktari zaonyesha ya kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliendelea kupata nafuu pole pole akielekea kupona kikamilifu. Majeraha yake yote yakapona isipokuwa jeraha la panja la kuume likawa kidonda kisicho kauka. Alijilazimisha kupitisha mchana katika sebule yake kushughulikia kazi yake na kutimiza wajibu wake kadiri alivyoweza. Alitoa darasa na mara moja moja aliwatazama wagonjwa na kuwaandikia dawa. Tarehe 30 Januari, alimwita Makhdum Mian Muhammad Siddik aje na karatasi na vifaa vya kuandikia; akamwambia kusoma mara tatu aya hii ya Kurani Tukufu: "Je, hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu wanachosomewa? Bila shaka katika haya mna rehema na mauidha kwa watu wanaoamini (29:52);" na, akiisha fanya hivyo, akamwambia:

''Katika aya hiyo Mungu Ameeleza hatua zote za kusonga mbele kwa mtafuta ukweli. Anauliza: Je, Kitabu Tulichomteremshia Muhamamd s.a.w. hakitoshi kwa mahitaji yote ya waaminio? Ndani yake mna rehema na mauidha ya kila namna.

Natambua vizuri maonyesho ya kudra na kila namna ya kashfi, lakini baada ya ushahidi wa Mungu naona itakuwa utovu wa hali ya juu sana wa shukurani kukimbilia njia nyingine yoyote ya maendeleo ya roho. Naihesabu kuwa mchezo tu. Kumbukeni hiyo, nyinyi nyote. Kama wazo lolote kinyume chake likizuka nyoyoni mwenu baada ya mimi kuaga dinia, tafuteni mwongozo kutokana na hii: Hakuna nguvu ya kuondoa ubaya wala hakuna nguvu ya kuleta wema isipokuwa kwa Mungu Mtukufu Mkuu.

Tena, zingatieni ushahidi mwingine wa Mungu uliopo mwanzoni kabisa mwa Kurani Tukufu, yaani: Mimi, Mungu, Najua sana, Nahakikisha kwamba hiki ni Kitabu Kikamilifu, hamna shaka ndani yake. Ndio mwongozo kwa wamchao Mungu (2:2-3). Ndiyo kusema kwamba Kurani yatoa njia ya pekee ya kupata wema. Nawaambieni hayo nikielekezwa na Mungu. Imesimuliwa katika Hadithi ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa anatumia njia mbali mbali za kupata ulinzi wa Mungu, lakini baada ya sura mbili za mwisho za Kurani Tukufu kuteremka akaacha kila kitu na akafungamana na hizo tu.

Itaendela toleo lijalo, Inshallah

Jukwaa la Historia na Pitio la vitabu vya Jamaat

Na Yassin Shoo,
Dar es Salaam

Mwenyekiti wa Jukwaa Sadr Khudam Ally Hamisi Mbwambwa alieza sababu za kuanzisha kwa mara ya kwanza jukwaa hili la kupitia vitabu vya Jamaat na Historia ya Jamaat; ni umuhimu wa kujua na kufahamu vitabu vya Masihi Aliyehaidiwa a.s, Vya Makhalifa pamoja na vya Masheikh mbalimbali katika Jamaat kwani vinatupa msukumo mkubwa wa kuelewa imani yetu na usahihi wake mbele ya Mwenyezi Mungu pamoja na shabaha ya kuwa kwetu Waahmadiyya. Baada ya maelezo hayo mafupi alimkaribisha Katibu Mkuu wa Jumuiya Ahmadiyya Tanzania Bwana Seif Hassan kufungua na kuongoza maombi.

Katibu Mkuu alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana wa Taala kwa kutukutanisha hapa kwa ajili ya tukio hili kuu la kihistoria, akachukua nafasi hiyo pia kumshukuru Sadr Khudam na timu yake kwa kuandaa na kumualika katika tukio hili "Kwangu binafsi ni faraja kuthaminiwa kupata nasafi hii adhimu ya kuufungua na kuongoza maombi ya ufunguzi wa jukwaa hili la vitabu lililoandaliwa na Khudamul Ahmadiyya lakini kabla ya kufungua nina machache ya kueleza juu ya Pitio hili la vitabu vya Jamaat na ihistoria ya Jumuiya " katibu Mkuu Seif alisema.

Leo tunashuhudia historia najua wao Khudam wameanzisha wameandaa tu lakini hili liwe la wanajumuiya wa rika lote ndio maana wote tupo hapa kupitia kusoma vitabu, Kupitia historia ndio tunaweza kujua yaliyopita, yaliyopo na yajayo ndio tunaweza jua mustakabali wetu.

Lakini kwa Waislamu na hasa Waahmadiyyakupitia historia ya Uislamu, Tunafahamu aya za mwanzo kabisa zilizoshushwa kwa Hadhrat Mustafa Muhammad S.a.w zilihimiza kusoma, Historia ni kumbukumbu ya mambo yaliyopita, ukitafuta au ukikuta zimekusanywa ukazisoma na ukaweza kuzielewa zinaweza kukufunza jinsi ya kuishi kwa wakati uliopo, Historia utunzwa katika njia endelevu kwa kuhifadhiwa katika vitabu.

Ni kwa kusoma vitabu tu "tunaweza kumjua Mwenyezi Mungu ni nani?, haki zake ni zipi? Tunawezaje kumtafuta Mwenyezi Mungu, tunawezaje kuzifuata nyayo za Mtume Muhammad S.a.w ili tuweze kuwa karibu na Mwenyezi Mungu? Yote haya tunaweza kuyapata kwa kupitiakusoma vitabu na historia ya Uislamu,kusoma vitabu siyo tu hiari ni wajibu kwa Waahmadiyya."

Masihi aliyehaidiwa as ametuagiza tusome kwa kuvirudia vitabu vyake kwa uchache mara tatu na Masihi Aliyehaidiwa ana vitabu takribani themanini, tunalazimika kuvisoma kwa kuvirudia mara kwa mara. Akatumia fursa hiyo kuwashuru Ansarullah, Khudam na Atfal walioudhuria ufunguzi wa jukwaa kwani wote kwa pamoja tumejaribu kutekeleza maagizo ya Seydina Ahmad a.s. ya kusoma vitabu vyake. Kupenda historia lazima usome vitabu na kusoma vitabu lazima ujue historia Katibu alisema.

Kwahiyo katibu mkuu akaweka bayana changamoto zilizopo ili kuimarisha jukwaa hili alililiita mtoto "inabibidi tulilee kama mtoto ili akue vizuri" ni jinsi gani tutakavyo yapeleka mapenzi ya kusoma vitabu kwa jamii akimaanisha kila pembe ya Tanzania, akasema kazi yangu ilikuwa kufungua na kuongoza maombi ya ufunguzi wa jukwaa hili limefunguliwa rasmi leo siku ya Jumamosi tarehe 26 Machi 2011 na litakuwa Jukwaa endelevu ndani ya Jamaat, naomba mjiunge nami kwa maombi.

Baada ya Katibu Mkuu kuufungua, Mwenyekiti wa Jukwaa alichukua nafasi hiyo kumkaribisha Sheikh Bakri Abeid kutoa salamu kutoka kwa Wakil –A'la, kwani ni hivi karibuni Sheikh Bakri na Dr. Mwanga wametoka Pakistan kwa maana hiyo walipata bahati ya kukutana na Wakil –A'la, Sheikh Bakri alisema akiwa katika gari wakiwa wanajiandaa kwenda uwanja wa ndege na Dr Mwanga kurudi Tanzania ghafla akatokea Wakil –A'la, akamwambia nina salamu maalum kwa ndugu zangu wa Tanzania uzifikishe kwao.

Wakil –A'la, akasema Seydina Ahmad alikuja kuleta mapinduzi makubwa ya kiroho, haya mapinduzi ya kiroho yanapatikana katika vitabu vyake fikisheni ujumbe huu kwa Waahmadiyya wa Tanzania kwa kusoma vitabu vya Masihi Aliyehaidiwa a.s. Kwa hiyo nendeni mkafanye na mhakikishe vitabu vinasomwa na muwe mnavifanyia mitihani.

Sheikh Bakri alieleza kustaajabishwa kwake na salamu za Wakil –A'la, na Jukwaa hili lilioandaliwa na Khudam, Sheikh akasema jukwaa hili linafanana na salamu za Wakil –A'la, alizozituma; akawapongeza Khudam kwa kuwa "Active" na inaonekana mnapata mwongozo makhsusi toka kwa Mwenyezi Mungu. Hii inakuwa kama mlikuwepo pale wakati Wakil –A'la, anatupa salamu ni kama mmepata "Telepath" Wakil –A'la, anasema hivi na nyinyi huku mnafanya vilevile alichokuwa anafikiri Wakil –A'la,.

Hizi ndio salamu zenu toka kwa Wakil –A'la, nami naomba mpango huu makhususi usiishie tu hapa bali uendelee kwa kuwashirikisha kaya zote katika jamaat, Lajna, Ansarullah. Kuwe na wakati maalum majumbani wa kusoma vitabu kama ni baada ya sala ya alfajir au Insha basi familia zijiwekee utaratibu wa kusoma chapta moja au hata kurasa mbili au tatu kila siku Sheikh alimalizia hivyo.

Kabla ya kumkaribisha Muadhama Mahmood Khamisin Mubiru kutoa mada ya Historia ya Jamaat, Sadr alikuwa na machache ya kuelezea juu ya Jukwaa ni kama darasa, hivyo jukwaa si mkutano kuna tofauti ya jukwaaa na mkutano kwahiyo walioudhuria wana nafasi kubwa ya kuchangia mada kwa uhakika. Pia akaonyesha kukereka na uhaba wa watu katika Jamaat wanaokuwa na uelewa na historia ya Jamaat kuwa ni mtu mmoja tu Mzee wetu Mubiru "Toka nianze kuwa na ufahamu wa jumuiya mara zote inapohitajika historia ya Jamaat lazima asimame Mzee Mubiru, kuna haja watu wajitokeze waanze kujifunza toka kwake kuchota historia na hekima zake kwani kuna leo na kesho tusije anza kutafutana hapa baada yake" Sadr alisema.

Sadr Khudam akakumbushia agizo la Masihi Aliyehaidiwa as wana Jumuiya wawe wanatembea na kalamu na "Notebook" ili wawe wanaandika mambo yanayotokea katika mikutano ya Jumuiya na hafla kama hizi ili kutunza kumbukumbu kwa wakati ujao kwani yeye binafsi aliitwa Sultan –al kalaam. Karibu Mzee wetu Mahmood Khamsin Mubiru.

Alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, yeye alisema angependa kuzungumzia mambo mawili, Neema ya Mwenyezi Mungu tunaambiwa lazima tuidhihirishe, tunawajibu wa kuieleza, kuifahamu. Neema tulioipata sisi Waislamu wa jumuiya ya Ahmadiyya itakuwa ni dhuluma kubwa kama tutabaki nayo sisi tu, Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumkubali Masihi wa zama hii, ndio neema tulioipata tukawaelezee wengine waikubali au waikatae.

Nchini mwetu kwa wale wanaoelewa mwenendo wa siasa, Waislamu wamekuja juu kabisa nadhani wana haki siwalaumu hata kidogo, Wamekuja juu kwa sababu Uhuru wa nchi hii umetoka mikononi mwao ni kweli kabisa ndio neema Mwenyezi Mungu aliyowapa wanaidhihirisha, Wanaieleza na Wanaifafanua na Hekima ni mali ya mwaminio popote unapoikuta unapaswa uichukue. Nadhani na sisi Waislamu wa Jumuiya ya Ahmadiyya si ajabu tuna mchango mkubwa zaidi na uhuru wa nchi hii kuliko wote wanaodhani hivyo, Kwahiyo tusione aibu kueleza, tufafanue juu ya nini tumeifanyia nchi hii.

Jambo la pili, jamii lazima ielewe ilipotoka, ilipo na inapokwenda natoa rai uwepo mpango maalum kama utakubaliwa tungeanzisha Chama cha wanahistoria wa Kiahmadiyya. Na kazi yake itakuwa kuratibu, kuandika, kueleza kufafanua kwa hakika. Yapo mambo yanaonyesha kwanini tunahitaji jambo hili Akakionyesha kitabu cha Centenary Khilafat Ahmadiyya alisema: Hiki ni kitabu chetu muhimu kimetolewa na Jumuiya ya Waislaamu Ahmadiyya bila shaka kimeandikwa na binaadamu yapo makosa ya msingi hayatakiwi niyaone mimi au yule bali tunatakiwa tuyaone wote kwa ujumla wetu.

Kwenye kitabu hiki kuna maelezo kwamba Sheikh Amir Abeid alikuwa Waziri kwanza ndio akatoka akaenda kuwa Mbashiri lazima tuelewe sisi tuna maadui wengi hata ulimi ukuteleza unaleta rabsha! Pia kuna jambo lingine kwenye kitabu hiki kinaonyesha Sheikh Amir Abeid alizikwa Tabora. Kwahiyo mimi nadhani tunajukumu kubwa sana ya kuweka mambo sawa sawa ili tusiwape wale ambao si marafiki zetu nafasi ya kutunyooshea vidole Muadhama alitanabaisha.

Kuna jambo moja la msingi nabii Ibrahim alifanya maombi kwa Mwenyezi Mungu wainulie mtume miongoni mwao atakaye wafundisha kitabu na hekima; mwaminio anapofanya jambo lazima ajue hekima na busara, lazima tujiulize tuna busara gani ya kukusanyika hapa kujua historia ni nini?

Historia inatuonyesha Papa wa Kikatoliki alikuwa na nguvu kubwa sana duniani lakini mipango ya Mwenyezi Mungu ya kumleta Masihi wake, nguvu hizo za papa zilianza kupungua kidogo kidogo ili kumpa nafasi Masihi Aliyeahidiwa kufanya kazi yake. Historia inaonyesha mnamo mwaka 1776 Marekani ilifanya mapinduzi ya kumuondoa Muingereza, baada ya mapinduzi wamarekani wakatangaza wao hawafungamani na Papa na watajiongoza bila kufuata mafundisho ya Papa. Mapinduzi ya 1789 ya Ufaransa nayo pia yalimpinga Papa kwa madai kuwa alikuwa ni sehemu ya waliokuwa wanawanyanyasa.

Muadhama aliendelea kueleza umuhimu wa historia: akasema usijali uwingi wa miaka bali unganisha matukio utapata jibu ya miaka hiyo na hali halisi ilivyo.

Jambo lingine ni kusambaratika kwa Ufalme wa Ottoman wa Uturuki ambao uliziunganisha baadhi ya nchi za Afrika ya kaskazini, Mashariki ya kati na Ulaya. Hii yote kama utaiangalia historia kwa jicho la kiuchamungu basi ni lazima utatambua kuwa ilikuwa ni mipango ya Allah kuvunja nguvu zilizokuwepo duniani ili Masihi wake aweze kufika na kufikisha ujumbe kwa binaadamu.

Lakini mwaka 1813 Ufalme wa Uingereza walipitisha sheria ya uhuru wa kuabudu kwahiyo haikuwa lazima mtu kuwa mfuasi wa Papa. Hii yote inaonyesha ni matayarisho ya kumpokea Masihi Aliyeahidiwa a.s., Mwaka 1815 kulianzishwa chama cha kuandika Biblia lakini kwa jicho la upande wa pili mwaka 1914 kulivumbuliwa mashine za uchapaji zama ambazo Masihi Aliyeahidiwa a.s Sultanul Qalaam alikuja kuvunja misalaba kwa njia za hoja na vitabu na siyo kutumia shoka kama wengine wanavyodhani. Mwalimu alieleza kuvunja misalaba maana yake siyo kutumia mapanga na mashoka bali ni kwa fikra, hekima na hoja madhubuti.

Historia yote hii, huwezi kupata kwingine zaidi ya kusoma vitabu kwahiyo ni jukumu letu sote kuhimizana kusoma vitabu vya Jamaat. Ndani ya kusoma tunaweza kuhifadhi kumbukumbu ambayo ndio huwa historia. Mwalimu Mubiru alimalizia mada yake.

Mwenyekiti akiahirisha jukwaa hilo alitoa mfano kuwa leo tunakipitia (Tumepitia) kitabu cha Hakika ya Ahmadiyya hata kama utakisoma mara mia unaweza usikielewe lakini ili uweze kukielewa barabara kitabu hiki itabidi usome tena kitabu cha Khalifa wa pili Hadhrat Mirza Bashirudin Uislam na dini nyingine. Kwahiyo ni kwa njia hii ya Jukwaa la Vitabu na Historia ya Jamaat tunaweza kujifunza mbinu nyingi za usomaji na uhifadhi wa historia, Kama tulivyosema awali huu ni mwanzo na kutakuwa na jukwaa lingine ambalo linaweza kusimamiwa na mwenyekiti mwengine siyo lazima mimi ili kuwa na Jukwaa endelevu ni wajibu wetu kuliendeleza kwa kupitia Tanzim zote kwani huu ni uhai wa Jamaat. Alimalizia kwa kutoa shukrani kwa wote walioudhuria ufunguzi wa jukwaa la patio la Vitabu na historia ya Jamaat.

Mwisho.

"Anta Minnii wa Ana Minka"

Kutoka Uk. 12

4, bab ul baai]. Katika Wahyi huu alioteremshiwa Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu Anasema kuwa anatokana na mtu asiye bakhili. Kama huwezi kusema kuwa bakhili ni mtoto wa Mungu vivyo hivyo si haki kung'ang'aniza kuwa Hadhrat Ahmad a.s. alikuwa tu na maana ya madai kuwa yeye ni mtoto wa Mungu au ana sifa za uungu.

Usemi wa aina hii hupatikana hata ndani ya Kurani Tukufu Sura Baqara:250 inaposema Man shariba minhu falaysa minnii yaani yeyote atakayekunywa maji katika chemchem hiyo basi huyo hatokani nami na Sura Ibrahim : 37 inasema Faman tabianii fainnahuu minnii yaani yule atakayenifuata basi huyo atatokana nami.

Halikadhalika Mtume s.a.w. aliwahi kutumia usemi wa aina hii kwa Hadhrat Ali r.a. pale alipomwambia Anta minnii wa Ana minka yaani wewe watokana nami na mimi natokana nawe [Mishkaat bab un naaqib uk 564 na Bukhari jal 2 Kitabus Swulh, bab kaifa yuktabu hadha].

Pia aliwahi kuwaambia watu wa kabila la Ash'ari kwamba; Hum minni wa Ana minhum yaani wao watokana nami na mimi natokana nao [Bukhari jal. 3 uk. 4 Bab quduumul Ash'arain qiswah Uman wal Bahrain na Tirmidhi jal 2 uk 234 Mujtabai Press na Bukhari jal. 2 uk 47 kitabul madhwaalim bab shirkat fit twa'aami].

Kuna Hadithi nyingine ya Mtume s.a.w. isemayo : 'Al 'Abdu minal Laahi wa Huwa minhu.' Yaani Mja au Mtumwa anatokana na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu Anatokana naye. [Baihaqi fi sha'abil iimaan, kwa hawala ya Jaamius swaghiir cha Imam Suyutwi, bab ul 'ain, jal 2, uk 68, chapa ya Misri].

Pia kuna riwaya nyingine isemayo: 'Abu Bakrin minnii wa ana minhu' Abu Bakar anatokana nami na mimi natokana naye. [Firdausil Akhbaar Deilmii, kwa hawala ya Jaamius swaghiir cha Imam Suyutwi, bab ul alif jal 1 uk 6].

Hadithi nyingine inasema : 'Innal Abbaasa minnii wa ana minhu' yaani Kwa hakika Abbas anatokana nami na mimi natokana naye. [Masnad Imam Ahmad bin Hanbal kwa hawala ya Kunuuzul Haqaaiq fii Hadiithil khairil khalaaiqi kilichoandikwa na Imam Abdur Rauful Munaadii, bab ul alif kwa hashiya ya Jaamius swaghiir, jal 1 uk 65 chapa ya Misri].

Hadithi nyingine inasema: "Banu Naajiyatin minnii wa Ana minhum" yaani Banu Naajiyatin wanatokana nami na mimi natokana nao. [Kunuuzul haqaaiqi bab ul baai, kwa hashiya ya Jaamius swaghiir jal 1 uk 99].

Tafsiri ya Baidhaawi ikitoa maelezo ya Sura Baqara : 250 isemayo Man shariba minhu falaysa minnii yaani anywaye humo hatokani nami, inasema Laisa bimuttahidin bii yaani yule atakayekunywa maji hataungana nami.

Ndani ya fafanuzi za Hadithi imeandikwa kwamba; Qauluhuu hum minnii wa ana minhum yuraadu bihil ittiswaalu a'anii hum muttaswiluuna bii yaani mradi wake ni kuungana kwa maana ya kuwa karibu nami. [Hashiya ya Bukhari jal. 2 uk 629 chapa ya Haashmi Mirath].

Kwa hiyo maana ya wewe watokana nami na mimi natokana nawe ni hii tu kwamba mimi ninakupenda na wewe wanipenda na makusudio yako na yangu hayatofautiani.

Mashrti ya Baiat

Kutoka Uk. 12

duniani basi adhabu hiyo itakuwa ni kafara kwa ajili yake. Na yule aliyelegea katika kuitekeleza ahadi hii ya Baiat, halafu Mwenyezi Mungu Akamsitiri basi shauri lake liko mkononi mwa Mwenyezi Mungu. Akipenda anaweza kumuadhibu au kumsamehe.
(Sahih Bukhari – Kitabu manaqibul – Ansaari – Baab Wufuudul Ansaari Ilaa Nnabiyyi Bimakata Rabiat – ul – Uqbatu.)

Tena kuna hadithi nyingine ambamo Hadhrat Ubadah bin saamit (r.a). anasimulia ya kwamba, "Sisi tulifanya Baiat kwa Mtume (S.A.W) kwa sharti hili kuwa tutasikia na kutii katika hali ya faraja na dhiki, au katika furaha au huzuni, na wala hatuta gombana na wenye mamlaka juu yetu. Na popote tutakapokuwepo tutadumu katika haki na hatutaogopa lawama ya yeyote mwenye kulaumu.
(Bukhari kitabul-Baiati babul Baiat alas sam'i wattaati)

Umul Mu'mimin Hadhrat Aisha r.a anasimulia kuwa Nabii Mkarim (S.A.W) alikuwa akichukua Baiat ya wanawake kulingana na aya hii tukufu:-
Yaani; Ewe Nabii! watakapokujia wanawake waliosilimu na kutaka kufanya Baiat katika sharti hili kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawauwa watoto, wala hawatamzushia yeyote uzushi, wala hawatakuasi katika mambo mema, basi pokea Baiat yao na uwaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mrehemuvu. [Sura 60 Almumtahana aya 13]
Hadhrat Aisha (r.a) anasimulia kuwa Mtume (S.A.W) alipokuwa akichukua baiat, mkono wake wenye baraka ulikuwa haugusi mkono wa mwanamke yeyote isipokuwa mwanamke aliyekuwa ni mke wake.

(Sahih Bukhari – Kitaabul – Ahkaami – baabu Baiatin Nisa-i)

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Kutoka Uk. 12

mwaka 2010 katika Mkoa wa Morogoro inachukuliwa kuwa ni maandalizi ya ziara ya Mikoa mengine itakayojulikana baadae.Inshaallah. Katika Mikoa hiyo ambayo Sadr ametembelea amejitahidi kupitia Jamaat nyingi na kuonana na Khuddam wengi na kujua hali zao.

Safari ya mwaka huu katika Mikoa ya nyanda za juu Kusini ambayo ilianzia katika mkoa wa Iringa , Sadr Sahib aliendesha kikao saa nne ya usiku baada ya kuona khuddam waliokuwa wanamsubiri walikuwa na hamu ya kumuona kiongozi wao na kujua lililomleta japo kwa ufupi.

Baada ya kutoa salaam toka kwa Amir na Mbashiri Mkuu, Sadr Sahib alizungumzia juu ya taarifa ya Ijtmaa na kikao cha Shura itakayofanyika mnamo tarehe 17,18 na 19 ya mwezi wa sita katika viunga vya Jumuiya Kitonga Mjini Dar es Salaam. Ijtmaa ambayo itaanza tarehe 17 na 18 ambayo wajumbe wake ni Khuddamula Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya wote. Alisisitiza kuwa ni wajibu wetu na ni haki yetu kuhudhuria Ijtmaa kwani ndipo mahali ambapo vijana Kiahmadiyya tunakutana kwa pamoja na kushindana na kupimana viwango vyetu vya maisha ya kimichezo na kielimu na ni fursa nzuri ya kuimarisha uhusiano wetu na kuongeza mapenzi ya kidugu baina yetu, alisema. Alikumbusha tangazo lililo kwenye gazeti la Mapenzi Ya Mungu kwani linaeleza aina za mashindano ya kielimu ambayo inabidi tujiandae nayo ili kila mmoja aweze kushiriki. Inshaallah. Na alisisitiza mashindano ya kuhifadhi Qur'an Tukufu kwa Juzuu Amma na Tabaraka yatashirikisha Khuddam na Atfalul Ahmadiyya wote na kuwaomba tujiandae vyema kwani huenda mchuano ukawa ni mkali. Mashindano mengine kwa Khuddam ni Qur'an Tafsiri kwenye Suratul Baqara kuanzia aya ya kwanza hadi kumi na saba, aya ya mia mbili hamsini na sita hadi aya ya mia mbili hamsini na nane na aya ya mia mbili themanini na tano hadi aya ya mia mbili themanini na saba. Aidha shindano la hotuba lililobeba mada ya umuhimu wa elimu katika Islam, kughani shairi la Masihi Aliyeahidiwa liitwalo mazuri hasa ya hamu ambalo linapatikana kwenye kitabu cha Masihi Aliyeahidiwa, hadithi za Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) zilizopo kwenye kitabu cha kiunga cha watu wema. Kwa upande wa Atfalul Ahmadiyya mbali na shindano la kuhifadhi Qur'an Tukufu pia kuhifadhi hadithi arobaini za Mtume Muhammad (s.a.w) na maombi ya Mtume Muhammad (s.a.w) ambapo dua wakati wa kwenda kulala, dua wakati wa kuamka usingizini na dua ya kupata mapenzi ya Allah zitashindaniwa.



Bw. Ali Khamis Mbambwa Sadr Khuddamul Ahmadiyya akiongoza msafara wa kuvuka mto wakati walipomtembelea katibu wa tawi la Ibonde ambaye alikuwa mgonjwa.

Baada ya kumaliza Ijtmaa yetu siku itakayofuata ni ya kikao cha Shura ya tanzim yaani tarehe 19 ya mwezi wa sita. Alisema hiki ni kikao muhimu amabacho kinajadili na kupendekeza kwa Khalifa Mtukufu mipango mbalimbali ya Tanzim yetu kwa mwaka ujao na Huzur Anwar (atba) akiyaridhia yanakuwa ndio mpango wetu wa utekelezaji baada ya kupata baraka zake. Hivyo mambo yetu yote yanapitia kwenye kikao hiki cha Shura ambacho wajumbe wake ni Qaid wa tawi kwa mujibu wa nafasi yake ya kiuongozi na mjumbe mwingine anachaguliwa sawa na idadi ya wanatawi yaani wakiwa chini ya ishirini wanapata mjumbe mmoja ambae ataambatana na Qaid kwenye Majlis Shura. Sadr Sahib ameruhusu wasilizaji kwenye kikao hiki isipokuwa ikifika wakati wa kupitisha maamuzi yakayohitaji kupiga kura wao hawatahusika na zoezi hilo,alisema. Sadr alimalizia kwa kuwataka Khuddamul Ahmadiyya wote waandike ajenda za Shura na wazitume kwake kabla ya tarehe 30.05.2011 na kuwaomba ushiriki wao katika mipango ya Tanzim.

Aidha Sadr alifikisha maazimio ya Shura iliyopita na kuwaambia khuddam wote kuwa ndio mambo ambayo Khalifa Mtukufu aliyapitisha hivyo inabidi tuyatekeleze sote na kwa bidii. Majukumu hayo yanahusu Michango, Tabligh na Tarbiyat na taarifa za utekelezaji wake zitumwe kwake kila mwezi na yeye aweze kumtumia Khalifa Mtukufu. Alisisitiza mbele ya khuddam walioonekana kuwa wasikivu na makini sana.

Itaendelea toleo lijalo. Inshallah.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Rajab 1432 AH | Juni 2011 | Ihsan 1390 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Ni juu ya kila Mwislamu kusikia na kutii amri akipenda asipende maadamu haamrishwi kufanya maasi. Na akimrishwa kufanya maasi (dhambi) hapo hamna kusikia wala kutii. ***(Abu Dawud, Tirmidh, Inb Majah)***

Maana ya Ufunuo wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

"Anta Minnii wa Ana Minka"

WEWE WATOKANA NAMI NA MIMI NATOKANA

Na Sheikh Bakri Kaluta Morogoro

Masheikh hupenda kutoa shutuma dhidi ya Wahyi huu wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba iweje Mungu Aseme kuwa Yeye Anatokana na Hadhrat Ahmad a.s. na Hadhrat Ahmad a.s. awe anatokana na Mungu. Wengine hata hudiriki kusema kuwa hapa kuna madai kuwa, Mungu Apishe mbali, yeye Ahmad ni mtoto wa Mungu na wakati huo huo Mungu ni mtoto wake.

Hadhrat Ahmad a.s. aliyeupokea Wahyi huu, mwenyewe anasema kuwa Wahyi huo uko katika lugha ya Istiara (fumbo) na sio ya dhahir (Haqiqatul Wahyi uk. 86 kwenye Hashia).

Katika lugha ya Kiarabu, usemi huu hutumika kumaanisha umoja na upendo.

Mtume s.a.w. akielezea kuhusiana na mambo matatu ya upole, khulka njema na utawa alisema: 'Thalaathun man lam takun fiihi falaysa minnii walaa minal Laahi' yaani yule ambaye ndani mwake hamtakuwa na sifa hizo tatu basi huyo hatokani nami wala hatokani na Mwenyezi Mungu. [Mu'ujam swaghiir twabraani uk 146].

Hapa haileti asilan maana ya kwamba yule ambaye ameepukana na sifa hizo tatu basi huyo si mtoto wa Mtume Muhammad s.a.w. na wala sio mtoto wa Mwenyezi Mungu bali atakayekuwa na sifa hizo basi huyo anakuwa ndio mtoto wao.

Mtume s.a.w. wakati fulani alisema: 'Ana minl Laahi 'azza wa jalla wal mu'uminuuna minnii, faman adhaa mu'uminan faqad adhaanii, waman adhaanii faqad adhl Laahu 'azza wa jalla.'

Yaani 'Mimi natokana na Mwenyezi Mungu na waaminio wanatokana nami, anayemuudhi mwaminio basi ameniudhi mimi, na anayeniudhi mimi amemuudhi Mwenyezi Mungu.' [Firdausil Akhbaar Deilmii uk 11, Hadithi hii ilisimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Jarraad r.a.]. Hatuwezi hapa kudai eti Mtume s.a.w. amedai kuwa ni mtoto wa Mungu na hivyo kuwa na sifa za uungu ndani mwake. Vivyo hivyo hakuna Sheikh yeyote yule mwenye haki ya kumzulia Hadhrat Ahmad a.s. madai kama haya kutokana na ufunuo unaofanana na huu.

Hadithi nyingine ambamo usemi wa aina hii umetumika ni hii iliyosimuliwa na Hadhrat Anas bin Malik r.a. kwamba Mtume s.a.w. alisema: 'Yaquulul Laahu 'azza wa jalla, Assakhiyyu minnii wa Ana minhu' yaani 'Mwenyezi Mungu Anasema Mkarimu anatokana nami Nami Natokana naye.' [Firdausil Akh-

Endelea uk. 11

Masharti ya Baiat

(HADHRAT KHALIFATUL MASIH WA TANO)

Na Sheikh Bakri Kaluta Morogoro

BAIAT NI NINI?

Jambo la kwanza kabisa ni hili kwamba Baiat ni nini? Nitatoa ufafanuzi wake kutoka kwenye Hadithi na kwenye nukuu za Hadhrat Masihul Maud a.s. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema: "Hii Baiat maana yake ya asili ni kujiuza, baraka na athari zake zimeambatana na sharti lile lile kama la mbegu iliyopandwa ardhini, hivyo hali yake ya mwanzo huwa hivi hivi kana kwamba iliyopandwa na mkulima na haijulikani kwamba sasa itakuwa nini. Lakini kama mbegu hiyo ni bora na ndani mwake mna nguvu ya kustawi, basi kwa fadhili za Mwenyezi Mungu na jitihada za mkulima huyo (mbegu) hiyo huchipua, na punje moja hugeuka kuwa punje nyingi sana. Halikadhalika mtu afanyaye Baiat kwanza hulazimika kuwa mnyenyekevu na kuachana na kujipenda na ubinafsi, hapo ndipo anakuwa mwenye uwezo wa kustawi. Lakini yule aliyefanya Baiat na kuendelea kuwa mbinafsi huyo hatapata baraka asilan. (Malfudhaat jal. 6 uk. 173).

Muradi wa Baiat ni kuikabidhi Nafsi kwa Mwenyezi Mungu

Kisha anasema: "Mradi wa Baiat ni kuikabidhi nafsi kwa Mwenyezi Mungu, mradi wake ni huu kwamba leo sisi tumeiuza nafsi yetu kwa Mwenyezi Mungu. Hii si sahihi kabisa kwamba hatimaye mtu anaweza kupata hasara kwa kutembea katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mkweli hawezi kamwe kupata hasara. Hasara ni ya yule aliye mwongo, avunjaye Baiat na ahadi aliyoifunga na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya dunia. Mtu yule atekelezaye mambo hayo kwa ajili tu ya kuihofia dunia, basi na akumbuke kwamba wakati wa mauti hakuna mtawala wala mfalme yeyote atakayeweza kumuokoa. Yeye ni mwenye kwenda tu kwa Hakimu wa mahakimu wote Atakayemuhoji kwamba kwa nini hukunijali? Hivyo ni muhimu kwa kila mwaminio kwamba amuamini Mwenyezi Mungu Aliye Mmiliki wa Mbingu na Ardhi na afanye toba ya kweli." (Malfuudhaat jal. 7 uk. 29 – 30).

Kutokana na maagizo haya ya Hadhrat Masihul Maud a.s. ni wazi kwamba Baiat ni kitu gani. Kama kila mmoja wetu alifahamu jambo hili kwamba dhati yangu sasa sio tena dhati yangu, sasa tunapaswa kushikamana, kwa hali yoyote ile, na maagizo ya Mwenyezi Mungu. Sasa tunapaswa kuyafuata na kila tendo letu liwe kwa ajili ya kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Hivyo huu ndio muhtasari wa masharti kumi ya Baiat.

Sasa ninatoa Hadithi mbali mbali ambamo maneno tofauti yanapatikana kuhusiana na Baiat.

Ai dhullah bin Abdullah anasimulia kwamba : "Ubada bin Swaamit alikuwa ni miongoni mwa wale Masahaba walioshiriki katika vita vya Badri na aliyeshiriki katika Baiat ya Uqba. Ubada bin Swaamit alimwambia kwamba Mtume s.a.w. alilisema jambo hili katika wakati ule alipokuwa amezungukwa na kundi fulani la masahaba, kwamba 'Njooni mfanye Baiat yangu kwa sharti hili kwamba

Yaani hamtamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hamtaiba, wala hamtazini, wala hamtawaua watoto wenu, wala hamtazua uzushi na wala hamtaniasi katika jambo lolote lililo jema.

Basi miongoni mwenu atakayetimiza ahadi hii ya Baiat basi ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Na yule atakayelegea katika kuitimiza ahadi hii na akapata adhabu humu humu

Endelea uk. 11

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Na Swaleh Kitabu Pazi, MBBS. Dar es Salaam.

Kwa mara nyingine tena Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania imepiga hatua katika maendeleo yake kwa kufanya ziara ya kihistoria katika mikoa ya nyanda za juu kusini ya Iringa, Mbeya na Ruvuma.

Ziara hiyo iliyoongozwa na Sadr wa Tanzim hiyo Bw, Alli Hamis Mbambwa kuanzia tarehe 09.05.2011 hadi tarehe 17.05.2011, ilikuwa na malengo ya kuwajulia hali vijana wa maeneo hayo ambao kama walivyo vijana wengi wa Tanzim hiyo walikuwa alikuwemo Mu'utamad (Katibu Mkuu) wa Tanzim hiyo Bw, Swaleh Kitabu Pazi, Muhtamim Mal (katibu wa fedha) wa Tanzim Bw, Issa Mwakitalima, Bw, Salum Ibrahim Ndatama ambaye ni khaddim toka Mkoa wa Dar es Salaam na Dereva wetu Khuddam aliyemaliza muda wake Bw. Chikulupi Kawinga.

Pamoja na mambo mengine Sadr alitumia ziara hiyo kuwafikishia Khuddamul Ahmadiyya mipango mbalimbali ya kitanzim iliyokwisha fanyika, inayofanyika na ambayo iko mbele yetu ili kila Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya awe na taarifa ya hali ya tanzim yetu kwa sasa na jukumu letu kama vijana kuhakikisha shughuli za Tanzim zinakwenda mbele zaidi na kwa kasi zaidi.

Ziara hiyo iliyofanyika mwaka

Endelea uk. 11



Picha ya pamoja kati ya Wanajamaat wa tawi la Songambele - Iringa na uongozi wa Khuddamul Ahmadiyya taifa wakati ulipotembelea tawini hapo.